# *Kurudi Na Yubile*

Asante, ndugu. Mwaweza kuketi. [Ndugu mmoja ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mwingine anafasiri—Mh.] Amina. Amina. Mungu asifiwe. [Ndugu mmoja ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mwingine anafasiri.] Amina.

2 Ni jambo zuri jinsi gani usiku wa leo kusikia hili likisemwa kabla tu hatujaninii . . . kabla sijaja kuwazungumzia, Mungu akituahidi kwamba atatupatia upako mpya. Hiyo ndiyo sababu tumekusanyika hapa, hiyo ndiyo sababu mkutano huu umeitishwa.

3 Bila shaka ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa usiku wa leo kukusanyika na kanisa hili tena, waabudu hawa, pamoja na rafiki yangu mwema, Ndugu Moore, mke wake mpendwa, na familia yao, na familia zote za Bwana zilizokusanyika huku kwa wakati huu wa ushirika, yubile. Tunakusanyika karibu na Neno la Mungu na penye sifa na ibada za watu Wake.

4 Na bila shaka ninakosa kitu kwa kutokuwepo hapa kumsikia ndugu yetu akizungumza juu ya kule kumwagwa, mwanzoni mwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika Mtaa wa Azusa huko Los Angeles. Nami nilitangulia kumtuma yule mtu wa kanda, Ndugu Sothmann, aliye hapa mahali fulani, kurekodi ujumbe asubuhi ya leo ili niweze kuusikia. Nasi tuliendesha gari jana usiku kupitia dhoruba, tukijaribu kuuwahi, lakini tukaukosa, nasi tukachoka sana, ikatubidi tu kusimama Little Rock yapata, kati ya saa sita na saa saba na kulala kwa muda kidogo, nililala kupita kiasi asubuhi ya leo. Kwa hivyo, kidogo tulikuwa wachovu, tumekuwa na shughuli nyingi sana, na kujiandaa sasa kwa ajili ya nchi za ng'ambo na kadhalika, kwa hiyo kidogo tulikuwa tumechoka. Na lakini, mimi ni . . . najua nitafurahia kusikia ujumbe huu wa mzee wetu juu ya wakati huo.

5 Siku moja huko, huko Canada nilipata fursa ya kumsikia Ndugu Moore akiisoma hiyo hadithi, nami sikuzote nimeshangaa kitabu hicho kilienda wapi, nilitaka kukisoma hicho, kuhusu huzuni na vilio vya watu hao katika kule kumwagwa mwanzoni kwa Roho Mtakatifu. Ninaamini mmoja wao alipoteza mtoto mdogo ama chochote kile, ilimbidi . . . hakuwa hata na jeneza la kumweka ndani, ilibidi aende kukata mbao kwa msumeno kutengeneza jeneza. Na loo jamani, jinsi walivyokataliwa na watu! Lakini hata hivyo, kwa imani isiyokufa, walisonga mbele kuona hili kanisa kuu siku hizi ambalo imezaa.

6 Inaonyesha kile ambacho imani inaweza kufanya. Nafikiri ikiwa mtu kamwe atakuwa na hakika moyoni mwao na ana kitu ambacho imani inaweza kutilia nanga, hawapaswi kamwe kukoma, haidhuru wameshindwa mara ngapi, wanapaswa kuendelea mbele.

7 Mnajua, kulikuwa na mtu siku moja ambaye alitaka kuandika ninii...alidhani angeweza kuandika katuni za vichekesho. Hakuna ambaye angekubali kipaji cha—chake, ndipo hatimaye akaanza kuandika tahariri ndogo kwa ajili ya kanisa, kisha akaingia katika maskini ge—gereji ndogo iliyojaa panya na kujaribu kuandika hadithi, wala hakuna mtu angezipokea, na kila gazeti likazikataa, kasema hakuwa na kipaji, lakini hata hivyo aliamini alikuwa nacho, naye akazidi kuendelea mbele. Ndipo akaanza kugundua upekee wa panya fulani ambaye alikuwa kwenye hiyo gereji, na hapo ndipo hadithi ya Micky Mouse ilipotokea. Naye Walt Disney sasa, mamilioni na mamilioni ya dola ambazo kampuni yake, au chochote alicho nacho, thamani yake, kwa sababu aliamini kwamba kulikuwa na kitu ndani yake, kinachodunda-dunda.

8 Na kama mtu anaweza kufanya hivyo kwa mambo ya kawaida, vipi kuhusu mtu ambaye amechochewa na Roho Mtakatifu, anayeamini kwamba Mungu anataka mafanikio Yake yaletwe kwa watu, naye atadumu na Maandiko?

9 Ninatazamia, juma hili, uamsho katika nafsi yangu mwenyewe. Nilimwambia mke wangu, jana, niliposikia habari njema, nami nikakimbia kule na kumkumbatia na kupaza sauti, "Niko huru!" kisha nikatoka nikaingia chumbani na kuanza kulia. Nami nikasema, "Unajua, na—na—na—nataka Mungu anipe uamsho ndani yangu mwenyewe." Nikasema, "Kwa takriban miaka mitano nimefinyiliwa na m—mzigo mkubwa ambao umeondolewa sasa na..." Nami nikawazia, "Loo, jamani, ninashuka kwenda kwa Ndugu Jack na kuwaomba watu wote waniombee ili nipate uamsho ndani yangu, ninauhitaji kweli." Nafikiri sote tunajisikia vivyo hivyo kabisa.

Dada Anna Jeanne, hakika ninapendezwa na makala hiyo uliyoandika, hasa juu ya kifuniko hicho kidogo, ningependa kukiona hicho.

10 Ninashukuru sana kumwona Dada Moore hapa, nikijua amekuwa mgonjwa kwa muda; naye Billy aliniambia ya kwamba alisimama hapa jukwaani muda mfupi uliopita kwa jambo fulani, lilikuwa ni ushuhuda wa neema ya Mungu, nguvu Zake za uponyaji.

11 Na mnamo wakati wa juma hili, Bwana akipenda, tunataka kuwa na ibada za uponyaji, kuwaombea wagonjwa, nasi tunakusudia kufanya hivyo, na kumwombea kila mtu, anayekuja kuombewa, nasi tunamtarajia Mungu atupe kumwagwa kwingine kwa Mtaa wa Azusa.

12 Na kwa hiyo sasa, najua . . . mmekuwa na . . . nilifikiri huu uamsho, ama, huu mkutano ulianza jana, lakini nikagundua umekuwa ukiendelea tangu Jumapili iliyopita, naamini. Kwa hivyo, najua mmekuwa na wazungumzaji wazuri humu, na bila shaka tunashukuru kwamba mkutano una hili . . . umeingia kwenye mazingira haya usiku wa leo. Haipaswi kuwa vigumu sana kufikiria jambo la kusema kwa kusanyiko sikivu kama hili, na—na Roho tayari yuko hapa, kwa hiyo unaingia tu moja kwa moja ndani Yake, unajisikia vizuri sana kufanya jambo hilo. Nami, ninashukuru kwamba siku zote ninapata jambo hilo hapa katika kanisa hili, ukaribisho mzuri wa Roho Mtakatifu.

13 Sasa, kuna watu ambao wamesimama, na huko nje, na ilikuwa ni wakati tuliposhuka kuja huku, walikuwa wakishuka kuja huku, wakifanya mstari wa kurudi; wao . . . hakuna nafasi ya kuingia orofa ya juu au kushuka chini, kwenye roshani na kadhalika. kwa hiyo, tu—tutajaribu kuharakisha tu upesi tuwezavyo, na usiku wa leo, kuzungumza nanyi kwa muda, halafu, kesho asubuhi, kuna ki—ki—kikao, naamini asubuhi. Nami ni—nina hakika kila mtu anataka kuwa hapa kesho alasiri, Ndugu Jack atajibu maswali.

Nikasema, “Ndugu Jack, vipi kuhusu hilo?”

Akasema, “Ni—ni—ninalo jibu, lakini sijui kuhusu swali lenyewe,” akasema. Kwa hivyo, hakika nina furaha kuwa mzigo uko juu yake kujibu maswali.

14 Sasa, tuna furaha na sikuzote tunapenda kukutana, na kuzungumza, na—na kuwa na wakati mzuri wa ushirika, na hivyo ndivyo ilivyo, lakini sasa hebu tutulie sasa kwa muda mfupi kwenye upande mwaminifu wa mambo haya, tukijua kwamba sote tunaandamana kuelekea mwisho, siku baada ya siku. Nilikuwa nikiwazia juu ya maskini mzee huyu hapa, kwamba ni wangapi walioabudu pamoja naye kwenye Mtaa wa Azusa tayari wameuvuka mto huo. Siku moja baadhi yetu, kama Bwana akikawia, tutakuwa tukizungumza kuhusu mikutano ya Shreveport kwenye yubile, tutakuwa tumevuka, wengi, inatubidi kukumbuka kwamba hatuna budi kufanya hivyo.

15 Kwa hivyo, inatupasa kuchukua kila tahadhari, hatutaweza kurudi na kujaribu tena, hatuna budi kulifanya sasa, kwa hiyo ninapokuja kwenye kusanyiko, sijaribu kamwe kuja kulifurahisha kusanyiko, sijawahi kuwa na hatia ya hilo, mimi huja kujaribu kumpendeza Mungu. Na wakati mwingine naweza kusema mambo na . . . ? . . . yanaweza kufinya au kuumiza, lakini silimaanishi kwa njia hiyo; tunahitaji kudumu na kweli na yaliyo mema, na kumwona Roho Mtakatifu akishuka na kuthibitisha hilo, ya kwamba ni kweli, na hilo ndilo tunalotafuta sote.

Sasa, kabla hatujasoma Maandiko, ningependa kama tukiinamisha tu vichwa vyetu tena kwa ma—ma maombi

mafupi.

16 Mungu wetu, tunakikaribia Kiti Chako cha Enzi, usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu. Kutamka tu Jina hilo kunatufanyia jambo fulani, kwa kuwa ni la kupendeza. Nasi tunakuja sasa, tukiinuka kutoka kwenye jengo hili dogo hapa, tukienda kupita kilele cha hili jengo, kupita mwezi, nyota, kuingia katika Uwepo Wako na kuyazunguka madhabahu Yako kuu ya dhahabu kuweka imani yetu na maombi yetu kule juu pamoja na Dhabihu yetu, Bwana Yesu, nasi tunakuja katika Jina Lake, tukijua ya kwamba Yeye alisema, "Mkimwomba Baba lolote kwa Jina Langu, nitawapa."

17 Na sasa tunakuja kwanza kuziungama dhambi zetu, na hatia zetu, na makosa yote, loo, ni, mengi sana, Bwana, hata ni kadhaa, lakini tunaomba tu rehema. Nasi tungeomba, Bwana, ya kwamba katika wakati huu mkuu wa ushirika, kwamba ungeturudia kwa umwagaji mkuu wa baraka Zako tena juu ya watu Wako. Tunapoona giza likitua na saa ikikaribia, na kuona makanisa yakizidi kutengana katika saa tunayoishi, utuvute karibu tena, Bwana, kwa vifungo vya ushirika karibu na Neno na karibu na Roho.

18 Jalia kusiweko na mtu ambaye sikuzote yu karibu, ndani au nje ya jengo hili, ila atakayefaidika usiku wa leo kwa kuja kwao hapa, na waje na mioyo iliyo wazi, na jalia sisi tunaozungumza, tuzungumze kwa mioyo iliyo wazi, na kwa jumla tukabidhiwe kwa Roho Mtakatifu, apate kutuchukua na kuyatenda mapenzi Yake.

19 Tunakushukuru kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya Ujumbe uliotolewa muda mfupi uliopita, hata tunahisi ndani ya mioyo yetu kwamba tunayo ahadi sasa kwamba—kwamba utatutembelea, nasi tunatazamia jambo hilo, Bwana, kama watoto ambao wamepewa ahadi.

20 Libariki Neno, usomaji, uyatakase masikio yasikiayo, na sauti inenayo, na uwalete zizini wale waliopotea, na wale waliobaki ndani, watie moyo hao waendelee. Mponye kila mgonjwa, Ee Mungu, jalia kusiwe na mtu mnyonge katikati yetu usiku wa leo ila atakayeponywa na Uwepo Wako. Na tutambue ya kwamba huu tunaouzungumzia na kusikia ukitujibu si kitu cha kubuni, bali ni uweza wa kufufuka kwake Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo, anayeishi miongoni mwa watu Wake. Tunaisikiliza Sauti Yako, Bwana, ili kusikia tunalopaswa kufanya. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

21 Sasa, ninawatakeni, mkipenda, mfungue pamoja nami katika Biblia kwenye Kitabu cha—cha Mambo ya Walawi mlango wa 25, nami ninataka kusoma kifungu cha 9 na cha 10 ili kutoa katika hili muktadha wa kile ninachotaka kusema.

22 Wakati mkifungua, nataka kuwatambua baadhi ya marafiki hapa ndani ambao ninawaona usiku wa leo: Ndugu na

Dada Williams kutoka Phoenix ambako mkutano unakuja hivi karibuni huko, pamoja na watu huko Phoenix; ninawaona pia Ndugu na Dada Norman hapa kutoka Tucson; moja kwa moja nyuma yao Ndugu na Dada Evans kutoka huko chini Georgia; na wengine wengi ambao nimeanza tu kuwaona na kuwatambua. Bwana awabariki.

Katika Mambo ya Walawi, mlango wa 25 na kifungu cha 9 na cha 10:

> *Ndipo baragumu ya yubile itapigwa kila mahali katika siku ya kumi ya mwezi wa saba, katika siku ya upatanisho mtaipiga baragumu katika nchi yenu yote.*
>
> *Na mwaka wa hamsini mtautakasa, na kutangaza uhuru katika nchi yote . . . wakazi wake:* nayo *itakuwa yubile kwenu; nanyi mtarudi kila mtu katika mali yake, nanyi mtarudi kila mtu kwa jamaa yake.*

23 Nami ninataka kuchukua somo kutoka: *Kurudi Na Yubile*. Sasa, kama ninavyoelewa, na nimeambiwa, ya kwamba hiki ni kipindi cha miaka hamsini iliyopita leo hii, naamini ndivyo, kama sikuelewa vibaya, ambapo Roho Mtakatifu alimwagwa upya katika jimbo la Louisiana.

24 Nami nimekuwa nikisoma historia kidogo juu ya mwenendo wa Kipentekoste, jinsi ambavyo miaka mia moja iliyopita hasa alimwagwa huko Urusi, wakamkataa, mnaona kile walichopata; na popote Mungu anapotuma baraka Zake na watu wakazikataa, mahali hapo sikuzote huingia katika machafuko, panaoza tu katika hali yake. Nasi tuna hakika ya kwamba huu Ujumbe na uweza wa Mungu, ambao sisi sote tunauamini, ni wa kigeni sana . . . wa kigeni sana kwa ulimwengu na njia yake ya kufikiria, mpaka, naamini, kwamba taifa letu limefanya kile ambacho wengine wamefanya. Sasa, kwa heshima na sifa za Mungu, tunashukuru kwa yale ambayo ametupa.

25 Nayo Israeli, Mungu aliwapa Israeli, ambao walikuwa mtumishi Wake, milki. Nasi tunataka kuliwekea msingi kama somo la shule ya Jumapili. Mimi, kesho usiku, ninakusudia kuhubiri juu ya somo la: *Sababu Na Jinsi Ya Kurudi*. Na sasa, usiku wa leo niliwazia ningeninii, takriban, ili watu wasilipate, wasilikose, hasa, kukosa kulipata, kidogo ningelifundisha kama somo la kile kilichotokea, na kwa imani yangu aminifu na safi, jinsi imekuwa, na kile kimetukia, na sababu yake. Halafu kesho usiku: *Tunarudije*?

26 Sasa, katika mfano, ama umbo, tunachukua Israeli kwa maana ni wakati wa yubile na Kanisa lilipewa sehemu, ambayo ilikuwa ni Kristo Mwenyewe aliyemiminwa na Roho Mtakatifu katika kila moyo ambao ungempokea na kufanyika wana wa Mungu. Sasa, Israeli walikuwa ni mtumishi wa Mungu, naye . . . walipewa milki, nayo milki hii haikupaswa kupewa mtu

mwingine yeyote, ilipaswa kuwa kwa Israeli pekee, Palestina ilikuwa ni mali yao.

27 Na kama tungekuwa na wakati, ama, wakati ungeturuhusu, hasa, kurudi nyuma na kuchukua kuzaliwa kwa wazee wetu hao (Walipozaliwa na hao wanawake, na, kila mmoja wakati mtoto alipokuwa akizaliwa, basi mama katika utungu wa kuzaa alitamka sauti ya mzee wetu huyu, ikamweka mahali pake, mahali pake, katika Palestina mamia ya miaka baadaye.) jinsi tunavyoweza kuweka imani yetu katika Neno hili la Mungu lililoandikwa kwa sababu limevuviwa sana, hata kila sehemu yake inashikamana, nayo inatuchorea picha ya kile Mungu alichokuwa, na kile Mungu alicho, na daima atakuwa!

28 Sasa, tunaona ya kwamba Yoshua alipowagawia urithi hao watu, kila mtu aliwekwa mahali pake, jinsi hasa akina mama hawa wa Kiebrania walivyowaita watoto hao, jinsi walivyowekwa kule Palestina katika mahali pao hasa: Asheri, Gadi, na—na Naftali, na kila mmoja, Yuda; kila mtu aliwekwa tu mahali pao.

29 Ni pi—picha ya ajabu jinsi gani inayotupa, kwa sababu ni mfano wa Mungu akiweka Kanisani, Mwenyewe, kila mshiriki, kila jiwe, kila mahali, kila Mkristo, kwake mwenyewe. Kila mmoja wetu kwa njia yetu ya kipekee ana mahali katika Nyumba ya Mungu, kama vile hekalu la Sulemani wakati lilipokatwa kote duniani, lakini lilipoletwa na . . . mpaka Yafa kwa, ikaelea majini, kisha ikachukuliwa kutoka huko kwa mkokoteni wa maksai, na mawe haya yote ya kipekee yalikuwa na mahali pake wakati hekalu lilipoletwa pamoja.

30 Nami nafikiri ya kwamba Mungu, kote kupitia wakati huu amechonga mawe ya kipekee ambayo huenda hatukuelewa, bali yana mahali pake hasa hekaluni, katika jengo la Mungu. Naye Yoshua, kwa uvuvio, sio kwa hisabati tu, yeye—yeye kwa . . . akivuviwa na Mungu alimgawia kila mmoja wa wazee hao katika mahali pao, jinsi hasa jina lao linavyostahili.

31 Ni pi—picha ya jinsi gani inayoweka mbele yetu ya Mungu katika kazi Yake kuu! Hakuna mtu angaliweza kulifanya ila Mungu, hakuna njia ya kufanya hivyo, Mungu pekee. Ilikuwa iwe ya mi- . . . ilikuwa iwe yao—yao milele, ilikuwa ni zawadi kutoka kwa Mungu. Mungu, kwa neema Yake ya ajabu, aliwapa watu hawa nchi hii katika mahali hapa na akawaweka humo sawasawa na Neno Lake na kuzaliwa kwa hao watu, kikamilifu tu, jinsi *ilivyoshikana* kabisa, nami nafikiri ilikuwa ni mfano.

32 Na sasa, hakuna mtu mwingine ambaye angeweza kuchukua mahali hapo, hapo palipaswa kuwa pa Israeli pekee, wao tu peke yao ndio wangeweza kuchukua mahali hapa, na bado zipo, baraka, mahali hapo. Na ikiwa *kwa namna moja ama nyingine,* katika zama hizi, kama walipoteza urithi wao kwa njia fulani, inaweza kuwa ni umaskini, inaweza kuwa ni njia nyingine

ambayo wa—walipoteza urithi wao ambapo baba zao...Mtu angemwachia mwanawe, angemwachia mwanawe, ilikuwa ni mali ya kabila hilo, ilikuwa mali ya watu hao milele, ilikuwa ni urithi.

33 Na kama sielewi Maandiko vibaya, ninaamini katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu Moja utakaokuja, mnajua ninachomaanisha, watarudi moja kwa moja mahali hapo, kwa maana tunajua Sayuni itaangaziwa, ule Mji mkuu, wala hawatakuwa na mchana wala usiku huko kwa kuwa hiyo—hiyo Nuru itaning'inia juu ya Sayuni, nami ninaamini katika Utawala wa Miaka Elfu Moja, makabila hayo yatachukua mahali pao tena.

34 Sasa, kama *kwa namna moja ama nyingine* mtu alipoteza urithi wake aliopewa na Mungu, ulikuja mwaka ulioitwa Mwaka wa Yubile, na huo ulikuwa, kila baada ya miaka saba walikuwa na ma—mapumziko, Sabato, kila baada ya siku saba walikuwa na sabato, kila baada ya miaka saba walikuwa na Sabato, na Sabato saba zilikuwa miaka arobaini na tisa, nao mwaka wa hamsini ulikuwa Yubile, na katika Yubile hii, kila mtu aliyepoteza urithi wake kwa njia fulani, kama alikuwa mzaliwa huru na Mwisraeli ukoo safi, haidhuru ni nani aliyeshikilia mali hiyo, ilibidi imrudie bure. Haikumpasa kulipa chochote, haikumpasa kufanya lolote, ila tu ni kuacha alichokuwa akifanya na kurudi kwenye urithi wake.

35 Loo, jamani! Alikuwa na haki yake, ilikuwa ni haki aliyopewa na Mungu, kwa sababu yeye, kwa neema, alikuwa ameirithi, nayo ingepewa baba zake na kupokezanwa mwaka baada ya mwaka. Haijalishi ni nini kilikuwa kimetukia, kama aliipoteza, lazima iachiliwe, ilimaanisha neema ni, njia iliyowekwa kwa kila mtu kurudi kwenye urithi wao halali.

36 Nayo inatupa picha ya jinsi gani usiku wa leo ya Kanisa katika siku hizi za mwisho! Unaona kile ambacho mwanadamu anaweza kufanya halafu unaona kile ambacho Mungu anafanya. Anachofanya mwanadamu kinashindwa, na kitashindwa, kimeshindwa, na daima kitashindwa, lakini kile ambacho Mungu anafanya ni cha Milele na lazima kidumu milele, hakuna kitu kinachoweza kukiondoa. Mungu alikitoa, ni zawadi Yake ya bure, na kwa uwezo Wake mkuu wa kuona mbele alikiona na kukiweka mahali pake, wala hakuna kitu kinachoweza kukisogeza kamwe, kiko pale Milele. Nayo Yubile ilikuwa njia ya Mungu ya kuonyesha neema kwa watu Wake kwa ajili ya kurejesha au kurudishwa kwenye nafasi yao halali.

37 Sasa, ninaamini ya kwamba hii ndiyo saa tena ya yubile, ninaamini ni wakati wa yubile. Ninaamini ya kwamba miaka hamsini iliyopita huko Louisiana, jimbo hili kuu ambamo Wapentekoste wana uweza na nguvu, ninaamini ya kwamba Mungu aliliweka Kanisa katika utenda kazi.

38 Nami sisemi hili kwa kukosoa, nasema kwa uaminifu, kwamba ninaamini ya kwamba ingawa hao washiriki Wapentekoste wachache wamekua wakawa makumi ya maelfu mara maelfu ya wafuasi mashuhuri, wenye nguvu, wanaohusishwa katika kila namna ya—ya serikali tuliyo nayo, na kila, kama vile polisi na—na watawala, na—na watu wakuu, hata katika serikali ya shirikisho. . . Siku moja nilifahamishwa kwamba wakati wa utawala wa Dwight Eisenhower, kwamba karibu asilimia arobaini ya wafanyakazi wa serikali walikuwa ama ni Wapentekoste au walikuwa na asili ya Kipentekoste.

39 Wazieni hilo, ndani ya miaka hamsini ambapo kanisa limekua kutoka kwa watu wachache huko kwenye Mtaa wa Azusa mpaka kufikia mojawapo ya makanisa yenye nguvu zaidi yanayosonga mbele ulimwenguni siku hizi. Tunashukuru kwa hilo, nami ninamshukuru Mungu kwa hilo, nami nina furaha sana kuwa mmoja wao, kwamba Mungu, kwa neema Yake ya ajabu, aliona inafaa siku moja kunileta ndani yao na kunifanya kuwa sehemu yao.

40 Wala kamwe sisemi neno hili lingine kwa ubaya wowote, bali ni kwa bidii ya kanisa: Lakini kanisa, hata hivyo, limeongezeka katika idadi, na limepata nguvu zaidi, limekua kifedha, lakini limeanguka kutoka jinsi lilivyokuwa siku ile, kiroho. Kumekuwa. . . Jambo kubwa zaidi ambalo lingeweza kuwapata, kama wakiwa na uwezo mkubwa kifedha, idadi kubwa, ama kama ikiwabidi kubaki katika uchache, jambo kuu zaidi ambalo lingewapasa kushikilia, lingekuwa ni Roho Mtakatifu yule ambaye Mungu, kwa neema Yake ya ajabu, alikuwa amewamiminia kuwaelekeza na kuwaongoza.

41 Ninaamini kwamba wamepoteza, na se—sehemu kubwa ya bidii hiyo waliyokuwa nayo, ule Moto uwakao ulioanguka na kuzishika roho zao, ambapo walienda pembeni mwa barabara, kwa njia za kando, na njia kuu, katika ninii, si kwa njia rahisi tunayosafiria siku hizi, bali kwa njia ya mateso, kupitia njia ya huzuni, kupitia njia ya majonzi, kukataliwa na kila mtu.

42 Jinsi ningependa usiku wa leo, kama ndugu yangu mwema labda anaweza kusikia katika ulimwengu mwingine. . . Lakini mtakatifu mmoja mzee, aliyeishi hapa Shreveport miaka mingi iliyopita, alikuwa akitokea, nilipokuja hapa mara ya kwanza, na kuniambia, “Ndugu Branham, unasema kweli kabisa, kanisa linapoteza mshiko wake. Loo, ninaomba kwamba Mungu atasaidia kulirejesha tena.”

43 Nami na Ndugu Lyle, tulipoketi huko, huyo ni baba ya Dada Moore, na jinsi alivyoniambia ya kwamba siku za mwanzoni, huko nyuma katika siku zile wakati walipoteswa na kufukuzwa kutoka kila mahali, kwamba alikuwa kwenye mkutano wakati mmoja ambako walikuwa. . . walikuwa wamewakataza kumwabudu Bwana katika Roho, ndipo kundi

la watu likaja na kufyatua risasi kupitia madirishani kwa bastola na bunduki, basi dada mmoja mkongwe aliyekuwa amesimama sakafuni huku ameinua mikono yake juu hewani, akimsifu Mungu, wakati madirisha yalikuwa yakishambuliwa kwa risasi kutoka kwenye bunduki, ndipo risasi hizo zikagonga nguo ya mwanamke huyo na kuanguka chini bila kumdhuru.

44 Tunahitaji kurejea kwenye nguvu za Mungu, na kitu *fulani* kinachoweza kufanya jambo lile lile leo. Ingawa katika idadi yetu. . .Mateso sikuzote hulitia nguvu kanisa; mambo yamekuwa rahisi sana kwetu, tunakuwa wavivu, tunafika mahali ambapo hatutaki kuendelea mbele, kwa sababu tumepewa tu kila kitu. Inahitaji huzuni, na machozi, na jasho, na maombi, na imani, na ahadi ili kusonga mbele katika uwezo wa Roho Mtakatifu. Ile bidii na nguvu walizokuwa nazo siku hizo zimetoweka kwa muda mrefu katika makusanyiko yetu. Nahofu kama madirisha yangepigwa risasi usiku wa leo, watu wangekimbia kila mahali wala wasingerudi tena.

45 Lakini. . .Na jambo lingine, ni vibaya sana, mwajua, kuwazia mambo hayo yakitokea hivyo, lakini hata hivyo ni, inathibitisha ya kwamba Mungu aliyekuwako katika siku za kale bado ni Mungu siku hizi, Mungu aliyekuwako, daima anabaki Mungu, Naye anawatarajia watu Wake ku—kutimiza nadhiri zao na ahadi zao, lakini tunapopata kila kitu kwa urahisi sana, basi tunateleza tu, na muda si muda mwajua, tumeyaacha mambo haya, tukapoteza urithi wetu.

46 Sasa, someni hapa chini, yapata kifungu cha 25, ama hapa ndani, katika huu 20, ama, mlango wa 25, hasa, wa Mambo ya Walawi, ambapo kulikuwa na kitu ambacho ningetaka kufananisha, si kwa kukashifu, bali kwa kiasi, kwa uchaji, na katika hofu ya Mungu, ambaye sote tuko Mbele Zake usiku wa leo. Je, mliona, mtakapokisoma mkienda nyumbani, kama hamjakisoma, kwamba mtu akinunua mali ndani ya mji wenye kuta, basi alikuwa na mwaka mmoja wa kuikomboa hiyo, kama aliiuza, na kama hakuikomboa hiyo, mali hiyo, kama ilikuwa ndani ya ukuta, ilibidi ibaki mle ndani, haingeweza kuachiliwa katika Yubile? Ilibidi ibaki mle, walikuwa upande wa pili wa ukuta, kamwe hawakusikia hiyo Yubile, baragumu ikilia. Walipiga baragumu wala isingeachiliwa.

47 Nami nahofia sana kwamba moja ya mambo ambayo tulikuwa nayo hapo mwanzo, jinsi watu wa kale walivyohubiri dhidi ya kujiundia madhehebu, tuligeuka na kufanya jambo lile lile ambalo baba zetu walipigana sana wapate kutoka kwake. Nao mji wenye kuta, ninahofu kwamba wengi wetu siku hizi, Wapentekoste wetu wengi sana wamezungushiwa kuta katika madhehebu fulani, mashirika fulani mahali fulani, wala hataisikia sauti ya yubile kamwe, kamwe hawataurudia ule—ule Urithi.

48 Sasa, kumbukeni, wale waliokuwa wamezingirwa na kuta kamwe hawakuwekwa huru, walikuwa watumwa wakati wao wote uliobaki, mwenye mali aliwamiliki kama waliweka urithi wao katika mji uliozingirwa na ukuta, lakini kama ilikuwa huko nje, miji midogo midogo ambayo haikuzingirwa na kuta, basi ilihesabiwa kama nchi tambarare, kwamba ingeweza kuwa huru katika Yubile.

49 Sitaki kukosoa, lakini ningependa tu kusema yaliyo kweli, ukweli wa Maandiko. Sasa, tunaona ya kwamba wengi wetu, katika siku hizi za mwisho, katika dhehebu letu la Pentekoste, kwamba tumeingia na kujiundia dhehebu, na kuukataa uongozi wa Roho Mtakatifu kwa hekima ya baadhi ya makundi ya watu. Badala ya kuwa na ushirika mmoja na mwingine, imetugawanya na kututenganisha katika mashirika mbalimbali ya watu, na kwa kufanya hivyo, imeuvunja Urithi wetu.

50 Sasa, kuta hizi, ndani, ambapo kama tutawahi kuzungushiwa kuta kufikia mahali ambapo hatuwezi kukubali Neno na Roho Mtakatifu, na ikatubidi kuchukua ka—kanuni za imani na kadhalika za kanisa badala ya nguvu za Roho Mtakatifu, yubile haitakuwa na maana yoyote kwa mtu huyo, la. Haijalishi ni kiasi gani unaweza kusema mama alikuachia ninii. . . Urithi wako, baba alifanya hivyo, lakini uliuza, na kuzingirwa kwa ukuta, na kuingia katika kanuni ya imani, na kukubali fundisho hili la sharti lililoingizwa kwenye ushirika wenu badala ya kuwa huru ndani ya Kristo na kumwacha Roho Mtakatifu atuongoze.

51 Huko nyuma kabisa katika wakati ambapo kanisa la kwanza lilikuwa likijikusanya pamoja, mara iliwabidi kujiundia madhehebu, na walipofanya hivyo, kwa sababu walihofia kwamba mtu mwingine angeanzisha, kiongozi, angechukua kundi dogo, walikuwa na maswala ambayo yaliibuka, ndipo basi ikawabidi kuyaundia madhehebu maswala haya, kama wangaliyaachilia tu, wamwache Roho Mtakatifu aondoshe, na kutoa, na kuelekeza ndani, na kuweka ndani, kanisa lingekuwa limeendelea mbele zaidi kuliko lilivyo sasa katika nguvu za kiroho. Naam.

52 Sasa, mtu na familia yake wangeweza kurudi kwenye urithi wao wa asili ikiwa wangeisikia Yubile, na sauti ya baragumu, na wajue ilichomaanisha kwao. Sasa, kama walimsikia kuhani akipiga baragumu (mhudumu, Baragumu ni Injili), na wanapoisikia, na wanajua maana yake, nao wanajua kwamba huo ni urithi wao, haidhuru waliupoteza wapi, walirudi nyuma umbali gani, chochote walichopaswa kufanya, walikuwa na fursa ya kuja na kuupokea tena urithi wao, familia nzima ingeweza kuja kuupokea urithi wao.

53 Ndivyo ilivyo usiku wa leo kwamba wanaume na wanawake, hapa Louisiana, wanaojua mambo tunayojua na wamesikia

kutoka kwa ndugu yetu na watu mbalimbali, juu ya ujuzi wetu wa Kipentekoste wa miaka mingi iliyopita, na wakakuta kwamba tumejijengea ukuta, ama, kama hatujajijengea ukuta mbali sana nalo hata hatuna budi kusikia kile mtu *fulani* anasema badala ya kile BWANA ASEMA HIVI kilivyo, na tunaweza kusikia Neno la Mungu linasema nini juu yake, sasa ni saa ya yubile, rudini kwenye Urithi wenu asilia, kwa Roho Mtakatifu halisi tena.

54 Kumbukeni, angeweza kuwa huru, haikumbidi kulipa chochote, haikumbidi kufanya lolote, ni kuamka tu na kwenda, hivyo ndivyo tu alivyopaswa kufanya, kurudi, kama alijua sauti ya baragumu, bali ilimbidi kujua sauti ya baragumu, mnaona, kwa maana walikuwa wana wa Mungu.

55 Sisi. . . Yesu alisema katika Yohana 8:35 kwamba Mwana hukaa nyumbani sikuzote. Sasa, mtumishi hakai, mtumishi hakai. Kumbukeni, yeye ni mwana, si mtumishi; iwapo yeye ni mwana, amezaliwa mwana, endapo ni mtumishi, ameunganishwa au amenunuliwa.

56 Loo, hakuna kitu kama kujiunga na Kanisa. Hakuna neno kwake katika Biblia. Huwezi kujiunga na Kanisa, Kanisa ni Mwili wa siri wa Yesu Kristo, ambao huna budi kuzaliwa ndani Yake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wala hakuna kitu kama kujiunga na Kanisa.

57 Katika Ufunuo mlango wa 17, kama utasoma katika *Diagloti*, *Diagloti Simulizi* ya muswada asilia wa Vatikani, utaona hapo katika Ufunuo 17, katika Toleo la King James, inasema, "naye alikuwa amejaa majina ya makufuru." Hilo kanisa kahaba, binti, alikuwa na binti, binti wengi walihusishwa naye, naye alikuwa ni kahaba, dini ya kwanza ya kimadhehebu iliyopata kuwako, iliundiwa dhehebu huko Nikea, Rumi, kule Nikea, baada ya Baraza la Nikea, ndipo ikawa dhehebu, kanisa la Kikristo la ulimwengu mzima la kimadhehebu, lilikuwa na binti.

58 Nanyi mnaona hapo toleo la King James linasema, "alikuwa na majina ya makufuru," lakini katika *Diagloti* asili, ilisema, "alikuwa amejaa majina yanayokufuru." Ni tofauti jinsi gani na "majina ya makufuru" na "majina yanayokufuru." Hiyo inamaanisha kwangu, sijui, mimi. . . kama nimekosea, Mungu anisamehe, lakini linamaanisha makanisa ambayo yamejitwalia majina ya Ukristo, yanayoishi kama ulimwengu, na kutenda kama ulimwengu, na kufanya mambo ya ulimwengu, na yameleta aibu juu ya Kanisa la kweli la Mungu aliye hai, nao wanajiunga na hao.

59 Unaweza kujiunga na chama cha Methodisti, chama cha Presbiteri, au chama cha Pentekoste, lakini huwezi kujiunga na Kanisa. Huna budi kuzaliwa ndani ya Kanisa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

60 Sasa tunaona mahali tunapofikia. Vema. Kumbukeni, wana hukaa, sikuzote wamo humo, wanaingizwa mle kwa kuchaguliwa tangu asili, Waefeso 1:5, "Alitangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hao ni wana waliozaliwa katika Kanisa la Mungu, nao daima wanabaki humo kwa sababu wamezaliwa ndani Yake. Hiyo ni kweli.

61 Mtumishi, sasa, kumbukeni, mtumishi hupata thawabu yake au ujira wake, lakini kamwe hakupaswa kuwekwa huru katika Yubile. Hapana, bwana. Mtumishi hakuwa huru katika Yubile ambaye hakuzaliwa Mwisraeli. Ilibidi azaliwe ili awe huru katika Yubile, alipata ujira wake.

62 Na watu wengi wanapata thawabu zao. Yesu alisema juu ya wanafiki, alisema, "Wana thawabu zao, lakini wewe ni tofauti." Naam, hivyo ndivyo Yesu alivyokuwa akisema katika Yohana 8 kuhusu Wayahudi. Walisema, "Tuko huru."

Akasema, "Watumishi hawakai nyumbani."

63 Lakini alipowazaa, hawakuwa watumishi tena, walikuwa ni wana na warithi pamoja Naye katika Ufalme. Hivyo ndivyo Kanisa lilivyo, ni warithi pamoja na Kristo katika Ufalme, warithi wa vitu vyote kwa Mungu, kupitia Kwake.

64 Sasa, tunaona ya kwamba kanisa lilienenda upande ule ule ambao mababu wake walipitia, ma—madhehebu ya kwanza ya makanisa. Imekuwa hivyo kote katika nyakati.

65 Lakini kamwe, kamwe, watumishi hawatakuwa huru, hawatalisikia Neno, hawataliamini Neno. Watumwa, walisikia sauti ya baragumu ikilia, huyo kuhani akipitia nchini, akipiga baragumu hii kwamba kila mtu alikuwa huru, ilisikika kote, uhuru kote nchini, na kila mtu aliyezaliwa Myahudi alijua angeweza kurudi kwenye urithi wake, sijali aliuzwa umbali gani, kile kilichotokea, angeweza kurudi, kwa sababu alizaliwa nyumbani, alikuwa nyumbani mwa baba yake, alizaliwa, lakini mtumishi hakujua alichokuwa akifanya. Loo, jamani!

66 Wote wawili walikuwa wakimfanyia kazi bwana yule yule, wameuzwa chini ya dhambi, Wapentekoste wengi usiku wa leo wanauzwa vivyo hivyo. Loo ndugu, rudini! Urudieni Urithi wenu asilia, nyote, geukeni mrudi, ni wakati wa kurudi.

67 Kafiri, sasa, mtumwa kafiri asingeweza kufanya hivyo, hakujua lolote juu yake, na hata hivyo, *kafiri* maana yake ni "asiyeamini," asiyeliamini Neno. Wengi wao watachukua mafundisho ya sharti na taratibu za ibada na kanuni za imani za kanisa badala ya kusikiliza Neno halisi, ndipo Neno halisi linapojitangaza, hawajui unachozungumzia. Wanataka kukuita mtakatifu anayejibingirisha, wanataka kukuita, kama walivyowaita wale mababu miaka hamsini iliyopita huko Louisiana, "wendawazimu." Kama ilivyokuwa huko nyuma katika siku za Paulo, "Kwa njia ya uzushi, ndivyo

ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu." Mnaona, kafiri hajui lolote juu yake, ingawa anadai kuwa kitu fulani, lakini hata hivyo, *kafiri* ni "asiyeamini," asiyeamini Neno la Mungu, hilo humfanya kuwa kafiri.

68 Ilikuwa ni kwa ajili ya wateule pekee, wateule wa Mungu, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, "Si yule apigaye mbio, wala yule atakaye, ni Mungu arehemuye." Mungu ndiye anayefanya jambo hilo, Mungu, kwa neema Yake. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Ni neema ya Mungu kwamba alilichagua Kanisa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

69 Kanisa hilo litalisikia Neno la Mungu, wataikataa kila kanuni ya imani, watalikataa kila dhehebu, kila dhehebu lililo kinyume, nao watamtumikia Mungu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Amina. Hakika wanajua sauti ya Baragumu. "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu."

"Unazungumzia nini?"

"Neno!"

"Unasema Hilo ni Sauti ya Mungu?"

70 "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Kondoo Wangu husikia Hiyo, wanaijua Hiyo, mgeni hawatamfuata." Hawasikii kanuni hizi za imani, hawasikii mafundisho haya ya sharti na mambo haya ambayo yameingizwa kuunda dhehebu badala ya mwili. "Mwili umeniwekea tayari," alisema Mungu, Matendo, au, Waebrania, "Mwili umeniwekea tayari. Dhabihu na matoleo hukutaka, lakini mwili umeniwekea tayari," mwili wa waaminio, mwili ambao umezaliwa.

71 Kabla ya kuwa mwili wa kibinadamu, kabla sijaweza kutenda kama mwanadamu, kabla sijaweza kutembea kama mwanadamu, kabla sijaweza kuzungumza kama mwanadamu, sina budi kuzaliwa mwanadamu. Fundo mtini lingejuaje jinsi nilivyotenda? Lingewezaje kusema, "Sitendi hivyo." Njia pekee lingeweza kuwa hivyo ni kuzaliwa kama mimi. Hivyo ndivyo madhehebu yalivyo, yamewavuta watu mbali, kwa maana yalifuata kanuni ya imani.

72 Lakini ili uwe mwana wa Mungu huna budi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, ndipo unakuwa kama Kristo na kufanya kazi za Kristo, basi wewe si wa kigeni kwa watu hao. Mwanadamu akitenda kama mwanadamu si jambo la kigeni; na Mkristo akitenda kama Mkristo, aliyezaliwa na Roho yeye yule, mnaona lile kundi la Kipentekoste hapo mwanzo, kundi lile lile la Kipentekoste linatenda vivyo hivyo kama limezaliwa na Roho yeye yule, maana limezaliwa. Ndiyo maana, siku hizi, kwamba watu hawalielewi Kanisa. Nalo Kanisa limeanza kuwa baridi

na la kawaida, likizifuatilia kanuni za imani na kadhalika na kuacha kumfuata Roho Mtakatifu. Vema.

73 Wengine hawajui sauti ya baragumu. Mtumwa amefungwa, Biblia ilisema hapa, kutoka kizazi hata kizazi. Kila mtu aliyeingia katika mji huo na kununua mali, alifungwa, hangeweza kukomboa mali yake katika yubile, haikuwekwa huru, wala asingeweza kuikomboa, ilibakia, yule aliyeinunua kutoka kizazi hata kizazi. Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema hapa, hana budi kubaki katika mji huo pamoja na mali yake, kwa maana huko ndiko urithi wake ulikuwa, ulikuwa katika mji huo. Hakuwa huru kurudi, kwa sababu alikuwa amejiuza, sasa, tunasema, kutoka kizazi hata kizazi.

74 Nilimwuliza mwanaume fulani muda si mrefu uliopita... Wakati mmoja, Daktari Bosworth, nadhani mnamkumbuka Ndugu Bosworth, alisema, "Nilimwuliza msichana mmoja usiku mmoja huko Toronto, Canada, 'Je, wewe ni Mkristo?'"

Akasema, "Ningetaka ufahamu, mimi huwasha mshumaa mmoja kila usiku." Kama...Mnaona, hayo ndiyo tu anayojua kuhusu Ukristo.

Nilimwuliza mwanamke mmoja wakati mmoja, kama alikuwa Mkristo.

Akasema, "Mimi ni Mmarekani, ningetaka uelewe."

Nikasema, "Hilo halihusiani nalo."

75 Nilikuwa ninaenda kumwombea mwanamke mmoja wakati mmoja, naye huyo mama akasema, "Vuta pazia hapo."

Nikasema, "Vema, nilikuwa nikitaka tu kuomba."

Akasema, "Vuta hilo pazia."

Nikasema, "Vema. Kwani wewe si Mkristo?"

Akasema, "Sisi ni Wamethodisti."

Nikasema, "Hiyo inashuhudia vyema kuwa wewe siye." Mnaona, mnaona, mnaona?

76 Angalia, kama ukisema, "Methodisti," hilo ni jina la makufuru tu; useme, "Mbaptisti," hilo ni jina linalokufuru tu. Tunaweza kusema, "Amina" kwa hilo, lakini ndugu, hebu nikuulize jambo fulani: "Na Pentekoste je?" Ikiwa si tukio la kuzaliwa mara ya pili, bado ni jina linalokufuru lililofananishwa na hapo mwanzoni...?...sahihi. Hiyo ni kweli. Mnaona, hawafahamiani, hawajui ushirika, yote wajuayo ni kanuni zenu za imani, wametulia tu kama namna fulani ya chama, kama vyama. Mimi...Vyama ni sawa ikiwa unataka kuwa mwanachama wake, lakini usikihusishe na Kanisa. Kanisa ni kundi la waaminio waliozaliwa mara ya pili walio katika Kristo kwa Roho Mtakatifu, wakiongozwa na Roho wa Mungu. Wao si wa ulimwengu, wako nje ya ulimwengu, wao ni tofauti na ulimwengu, hicho ndicho kinachowafanya kile walicho. Uhai

wao umekufa nao wamefichwa ndani ya Kristo na wamekufa katika Kristo na wamefichwa na, kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu, wako mbali na mambo ya ulimwengu.

77 Mtumwa aliyefungwa, kutoka kizazi hadi kizazi: Mwanamke mmoja alisema, "Vema, mimi ni Mlutheri." Vema. [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] (Samahani.) "Mlutheri, mama yangu alikuwa Mlutheri, babu yangu alikuwa Mlutheri." Vema, mtumwa kutoka kwa mmoja hadi mwingine, aliyepokezanwa moja kwa moja kuendelea, atabaki tu hivyo. Hutawahi kuwa huru katika yubile. Ungeweza kuhubiri Neno, ungeweza kuona Roho Mtakatifu akiwaponya wagonjwa, akifungua macho ya vipofu, kunena kwa lugha, kufasiri vile hasa Biblia inavyosema, lakini hujui sauti ya Baragumu. Kweli! Huo ndio ukweli. Hawajui sauti ya Baragumu, wamejiuza, waliweka Urithi wao kule nyuma katika mji fulani uliozingirwa kwa kuta.

78 Kanisa letu la Kipentekoste limefanya jambo lile lile, hasa, kuurudisha moja kwa moja katika mji uliozingirwa kwa kamba, hawalisikii Neno la Mungu. Wanasema, "Wasipokuja *hivi*, lisipokuja kwa kundi letu, vema basi si kitu sahihi, lakini jina lako haliko kwenye vitabu vyetu, huwezi kwenda katika Unyakuo."

79 Jina lako liko kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, nalo liliwekwa mle kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wala hakuna kitu kinachoweza kulifuta. "Kondoo Wangu waijua Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata." Naam, bwana.

80 Kama mtumishi tajiri...Mtu mmoja akiingia, akawa mtumishi na akawa tajiri, naye akamnunua ndugu, sasa, ndugu huyo angeweza kukombolewa na jamaa wa karibu, jamaa wa karibu angeweza kuja, amchukue katika mwaka wa Yubile, naye angeweza kumkomboa.

81 Ni Kristo wa kupendeza jinsi gani tuliye naye hapa, pi—picha nzuri, hasa, ya Kristo! Jinsi ambavyo m—msafiri huko nje kifungoni, aliyeuzwa kwa miji tajiri huko nje, aliyeuzwa katika utajiri wa madhehebu, lakini ndugu wa jamaa wa karibu ambaye anajua yuko huko nje, usiku fulani aweke Biblia yake chini ya mkono wake, na aende kumtafuta, jamaa wa karibu, kwa sababu ana roho ile ile, amezaliwa katika familia ile ile, aende akamwite atoke katika kundi hilo! Yeye ni mkombozi wa jamaa. Jinsi ambavyo hiyo picha ilionyeshwa vizuri sana katika Kitabu cha Ruthu: Boazi, hapo alipochukua mahali pa mkombozi wa jamaa, akimwakilisha Kristo!

82 Kanisa sasa ni kama Israeli. Kanisa ni kama Israeli walipotoka Misri. Wakati Israeli walipokuwa huko chini Misri, Mungu kwa neema Yake ya ajabu, bila madhehebu yoyote wala kitu chochote kingine, Aliwaita Israeli kwenye afya yake,

akawaita kwenye urithi wao. Yeye. . .Neema iliwapa nabii, neema iliwapa Nguzo ya Moto, neema ikawapa mwana-kondoo, mwana-kondoo wa dhabihu, neema ikawapa nguvu, neema ikawapa ukombozi, neema ikawapa ushindi, neema ikawapa mambo haya yote, nao wakacheza katika Roho, na kupaza sauti, na kumsifu Mungu juu ya jambo hilo.

83 Wala hawakujua walipokuwa wakicheza ukingoni mwa Yordani pale, ama, Bahari ya Chumvi, kwamba walikuwa umbali wa miaka arobaini kutoka kwenye hiyo nchi; walikuwa umbali wa kama siku tano tu, lakini walifanya kosa lao la kijinga katika Kutoka mlango wa 19 ambapo walikubali torati badala ya neema, ambapo waliikataa njia ya Mungu kusudi wajipatie njia wenyewe, "Tupe kitu cha kufanya." Hilo limekuwa wazo la mwanadamu wakati wote.

84 Sasa, kumbukeni, limekuwa ni wazo la mwanadamu, ni. . . hiyo ndiyo tabia ya mwanadamu. Adamu alionyesha hilo katika bustani ya Edeni, wakati alipopotea, badala ya kumrudia Mungu kwa ajili ya neema, alijaribu kujitengenezea mwenyewe nguo. Na tangu wakati huo amejaribu kuwa na kitu cha kufanya kwa ukombozi, wakati ukombozi ni toleo la bure la neema ya Mungu, Mungu peke yake. Hakuna unachoweza kufanya ili kujiokoa, Mungu alikuokoa. Hakuna njia hata kidogo unayoweza kufanya, lakini mwanadamu anataka kitu cha kufanya ndani yake; wanaikubali siku hizi.

85 Na kama miaka hamsini iliyopita, wakati mama zenu na baba zenu, ninyi Wapentekoste usiku wa leo, wakati hao wazee wa zamani, na huyu anayeketi mimbarani hapa usiku wa leo, walipopaza sauti na kumsifu Mungu, walitoka katika hayo madhehebu. Mbona, ukiwazungumzia kuhusu madhehebu, wangekucheka usoni pako, walikuwa huru. Naam, bwana. Walipaza sauti na kumsifu Mungu, walinena kwa lugha, walikuwa na ishara na maajabu na miujiza, Roho Mtakatifu akashuka, wakaiona sura halisi ya Kristo, wakafanya ishara kuu na maajabu, wakateseka, wakamwaga damu, wakaingia chini ya mateso, uchungu, na kila kitu kwa ajili ya huduma hiyo.

86 Na sasa walifanya nini? Jambo lile lile walilofanya Israeli, walifanya kosa lao la kijinga pia, walitaka kuunda dhehebu. Nalo lilifanyaje kwa Israeli? Lilifanya nini kwa Israeli? Hilo. . . Wa—wasingekubali uongozi wa Roho Mtakatifu, wasingekubali uongozi wa Musa, hata walijaribu kuwainua Kora na Dathani na kadhalika ku—kuwaongoza. Hawakutaka uongozi ambao Mungu alikuwa amewaandalia.

87 Na leo hii hatuutaki huo uongozi, ama kanisa halitaki, ambao Mungu ameandaa, wanajaribu kuwazia njia nyingine. Wanaenda kwenye seminari, wanawaelimisha watu wao, wanarudi wakiwa na ujuzi wa kitheolojia.

88 Loo, afadhali niwe na mtu anayenihubiria ambaye hajui ABC zake, ambaye hajawahi kuwa katika se—seminari ya theolojia, na awe na ujuzi huko ng'ambo kwenye kilima cha mafunjo mahali fulani nyuma ya kisiki na Mungu akamjaza Roho Mtakatifu. Bila shaka. Acha aongozwe na Roho, Mungu atafanya kila kitu kielekee moja kwa moja upande wake, yeye ni kama sumaku, huwezi kumficha, kama vile nyumba inayoteketea kwenye upepo mkali, huwezi kumzima, ataendelea kuwaka moto. Anawaka kwa ajili ya Kristo, huwezi kufanya lolote kulihusu. Naam.

89 Walifanyaje hata hivyo? Walifanya jambo lile lile ambalo Israeli walifanya. Loo, walipata ushindi, walipaza sauti, walicheza dansi, walinena kwa lugha huko Pentekoste, huku chini Louisiana miaka hamsini iliyopita, lakini kama vile Israeli walivyotaka jambo la kufanya wao wenyewe, vivyo hivyo na kanisa la Kipentekoste; wote wakaundia dhehebu Assemblies of God, kisha baada ya hao wakaja wengine, naamini wanaitwa United, ama, kitu *fulani*, kisha likaja lingine, kisha lingine, kisha lingine, kisha lingine, mpaka hebu angalieni lilipo siku hizi.

90 Mnajua mlilofanya? Jambo lile lile walilofanya Israeli. Walipoukataa mpango wa Mungu uliotolewa kwa ajili yao, walianza kutangatanga. Hivyo ndivyo kanisa limefanya leo, kutangatanga na kuingiza kila kitu katika dhehebu lao: wavuta tumbaku, na watu wasio watakatifu waliooa mara nne ama tano, na chochote kile, na kuwaacha wahubiri, na kumchukua mwimbaji mshamba huko nje kutoka kwenye ho—hospitali ya wendawazimu huko nje usiku mmoja na kumwacha acheze jukwaani kesho yake usiku. Mbona, ni fedheha kwa Kanisa la Mungu aliye hai kuwazia jambo kama hilo! Bila shaka.

91 Walifanya nini? Imeleta majina ya makufuru, ikatupilia mbali Pentekoste, jina lile lile linalopaswa kuwa takatifu, imewaanika hadharani kwa sababu wanasema, "Yeye ni mwanamume Mpentekoste, yeye ni mwanamke Mpentekoste, wao ni Wapentekoste, angalieni, jinsi wanavyofanya na kutenda." Hiyo ni kweli. Majina yanayokufuru! Hakika, huo ndio ukweli.

92 Naam, bwana, walifanya kosa la kijinga walipofanya hivyo, nao wakatanga-tanga kwa muda wa miaka arobaini, hivyo ndivyo walivyofanya hasa; walitangatanga kwa miaka arobaini wakati hawakuwa na zaidi ya siku tano kutoka kwenye nchi ya ahadi. Ni takriban maili arobaini kutoka Bahari ya Shamu hadi walipovukia Yordani, yapata maili arobaini; wangaliweza kutembea kwa siku tatu au nne na kuingia katika nchi ya ahadi, lakini walifanya chaguo lao wenyewe.

93 Nalo kanisa lingekuwa ni Kanisa usiku wa leo, tukufu, lisilo na waa wala kunyanzi, kama wale baba wangalikubali na kukaa na Roho Mtakatifu ambapo Mungu alikuwa amewatoa kutoka

katika hayo madhehebu, lakini walirudi moja kwa moja ndani yake kama mbwa kwenye matapiko yake na nguruwe kwenye kugaagaa kwake, walirudi moja kwa moja tena ndani yake, na sasa tumetangatanga miaka mingine hamsini, tukizurura nyikani.

94 Lakini ilifika wakati ambapo Mungu alisema, “Mmekuwa kwenye mlima huu kwa muda mrefu kutosha. Njoni, tunavuka.” Na liwe ndilo tukio la Louisiana sasa katika yubile hii. Na liwe tukio tena kwamba Mungu, Roho Mtakatifu, atasema na watu wa kizazi hiki, wana wao, kama walivyofanya huko nyuma wakati wale wapiganaji wa kale wamekwisha kufa, waliopiga vita, na kusema, “Je, wewe . . . Nenda ufanye *hivi*, nitafanya *hivi*. Na kama ukibatiza katika Jina la Yesu, hatutakuwa na uhusiano wowote nawe. Nawe ukifanya *hivi*, tutakuwa na *hilo*, na jambo hilo *lingine*.” Hao wapiganaji wa kale wamekufa. Hiyo ni kweli.

95 Ni wakati wa kuinuka, iweni wana wa Mungu katika Jina la Yesu Kristo, na mwinuke kufikia mahali fulani ambapo mnaweza kurudi katika yubile hii na kusikia sauti ya Baragumu ya Injili ya Neno la Mungu. Ninyi ni ndugu, hamjajiundia dhehebu; ninyi ni ndugu kwa sababu hamwezi kuundiwa dhehebu, mmezaliwa wana wa Mungu. Ikiwa watumwa wanataka kukaa katika mji wenye kuta, waache wakae, lakini ninyi mko huru. Amina. Mko huru. Hebu turudi, turudi kwenye Urithi wetu, hima turudi kwenye mwanzo, turudi kwenye “wao wana—wanaongozwa na uvuvio wa Roho Mtakatifu.”

96 Hivyo ndivyo walivyokosea. Wakati mmoja tena Israeli walifanya hivyo. Ni jambo tu ambalo watu hufanya. Wakati mmoja Israeli walitazama pande zote baada ya kugawiwa urithi wao, walitaka kuwa kama walimwengu wengine, walitamani mfalme.

97 Nabii mzee . . . Manabii sikuzote wamekuwa njia ya Mungu ya kuwaambia watu, “Neno la Bwana liliwajia manabii.” Nabii ndiye aliyewaambia ukweli.

98 Basi Samweli alisimama, akasema, “Je, nimewahi kuchukua pesa zenu, ama nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana isipokuwa lile lililotimia?”

99 Wakasema, “Hiyo ni kweli, hujawahi kuchukua pesa zetu, hujawahi kuchukua riziki zetu, hujawahi kutuomba vitu, wala hujapata kutwambia lolote katika Jina la Bwana ila ukweli.”

Akasema, “Basi achaneni na mambo hayo huko nje. Ati mjipatie mfalme juu yenu? Mungu ndiye Mfalme wenu.”

100 Nalo halikumpendeza Mungu. Samweli akalia mbele za Bwana, naye Bwana akasema, “Hawajakukataa wewe, Samweli, wamenikataa Mimi, wewe ni chombo tu ninachofanyia kazi, acha wawe naye.”

101 Na huyo ndiye waliyempata hasa, nasi tunaona huzuni iliyofuata hilo, Mungu ndiye Mfalme wao. Mungu ndiye Mfalme wetu, Roho Mtakatifu ndiye Kiongozi wetu, Mungu utupe Roho Mtakatifu, jalia tukae Naye: Biblia ya kuelekeza ili kuona kama ni Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hawezi kuahidi kitu fulani *hapa*, akikane *hapa*, hana budi kudumisha yale hasa aliyosema apate kubaki Mungu. Kweli. Hana budi kudumu Roho Mtakatifu, hana budi kuwa yule yule. Naam. Walitaka kutokumwamini Samweli wakati Samweli alikuwa na Neno la Bwana na aliwaambia.

102 Israeli walipaza sauti na kucheza, hakika walikuwa na wakati mzuri sana, lakini waligundua, walitangatanga kwa miaka arobaini. Sasa, katika kutangatanga kwetu... Je, uliwahi kuwazia walichofanya kule nyikani? Uliwahi kuwazia kile Israeli walifanya? Mungu aliwabariki. Hakika aliwabariki. Walikuwa na mabustani yao, mazao yao, walioa wake zao, wakawalea watoto wao, Mungu aliwabariki. Naye ameubariki mwenendo wa Kipentekoste. Yeye...Hakika. Lakini kumbukeni, hilo silo ambalo Mungu aliwatumia huko, kuishi katika nyika lile, walikuwa wapite tu nyikani, walikuwa njiani kuelekea nchi yao ya ahadi.

103 Kanisa lilipaswa kuendelea hadi kwenye ahadi kamili, Kanisa usiku wa leo linapaswa kuwa katika fahari Yake ya utukufu, linapaswa kuwa likikusubiri Kuja kwa Bwana, badala yake, limetawanyika kila mahali, likishangaa ni *upi* ukweli, "Je, *hii* ni kweli? Je, *hiyo* ni kweli? Nitajiunga na *hili*, kisha niende *huku*, na kushuka chini *kule*." Loo, rudini, yaondokeeni mambo hayo.

104 Sasa, imetufanyia nini? Iliwafanyia hivyo, iliwafanya kubaki nyikani. Imeturudisha moja kwa moja kwenye matapiko tulimotoka, tulijiundia madhehebu, nayo yakaturudisha moja kwa moja kwenye matapiko yale yale tulimotoka. Kwani hamwezi kuelewa ya kwamba Mungu hakuwahi kuwa na dhehebu, kamwe hakutawaza moja, wala kamwe hakunena juu ya moja, lakini sikuzote aliyapinga? Mungu anataka kuwaongoza watu, watu hawawezi kujiongoza wenyewe. Wanasema, "Tuko kwenye wingi wa mashauri."

105 Hilo lilithibitika kuwa ni bandia wakati mmoja wakati Yehoshafati aliposhuka kwenda kukutana na Ahabu, nao wakasema, "Inatupasa...Tutamtaka Bwana shauri tu." Lilisikika la Kimaandiko sana, lilisema, "Kuna Ramoth-Giliadi, ni mali yetu, Mungu alitupa sisi. Watoto wa Kiebrania wanapaswa kuwa wakila hiyo ngano kule juu, lakini badala yake adui anaila. Je, hamfikiri tunapaswa kukwea huko juu?"

106 Naye Yehoshafati akasema...Mtu mzuri akishirikiana na wabaya, hivyo ndivyo makundi ya Kipentekoste yalivyo usiku wa leo, watu wazuri, Wamethodisti, Wabaptisti, na kadhalika,

Pentekoste sio dhehebu, Pentekoste ni tukio. Mnaona? Watu wengi wazuri waliingia kwenye kundi baya, wakisikiliza mafundisho hayo ya sharti na kulikataa Neno. Hiyo ni kweli hasa.

Angalieni, Yehoshafati alisema, "Je, haitupasi kumtaka Bwana shauri?"

107 Akasema, "Hakika, samahani, loo, bila shaka, nilipaswa kujua jambo hilo. Ninao manabii wazuri mia nne wa Kiebrania hapa chini, nitashuka niende niwalete."

108 Kwa hiyo, akashuka, wote wakatabiri, Zedekia akajitwalia pembe mbili, akasema, "Kwea." Hakika, linasikika lenye mantiki. Wakasema, "Mungu alitupa hiyo nchi, hiyo ni yetu." Lakini kuna jambo linaloambatana nayo, hamna budi kumtii Mungu mpate kukaa katika nchi hiyo.

109 Ndivyo ilivyo usiku wa leo, Pentekoste, mlimwasi Mungu mlipojiundia dhehebu na kujitenga, mnaonekana hamna imani. Unaweza kuwa Mpentekoste, lakini wewe si . . . kwa jina, lakini huna budi kuwa Mpentekoste chini ya masharti: kwamba Uzima wa Kristo, Neno la Mungu, linaweza kutiririkia ndani yako na kujidhihirisha, na kuthibitisha ni, kuwa ni Mungu, na Mungu akitenda kazi kupitia kwako, Uzima wa Kristo ndani yako.

110 Sasa, tunajua hilo . . . Angalieni kile hii . . . Yeye alisema, "Naam, ninii . . ." Wote wakasema, "Kwea, Bwana yu pamoja nawe. Kwea ukawasukume nyuma watoke nchini, ni mali yetu."

Nanyi mnajua, hilo halikuonekana sawa kwa Yehoshafati, alikuwa mtu wa kiroho. Akasema, "Je, hakuna mwingine mmoja ambaye tungeweza kumtaka shauri?"

111 "Kwa nini kumtaka shauri mmoja wakati hapa kuna dhehebu zima, sasa, pamoja na maaskofu wote na wazee wa jimbo na wote? Wote wamesimama hapa nje. Kwa nini kumchukua mwingine?"

Akasema, "Lakini hakika, kuna mmoja zaidi."

112 Akasema, "Naam, ninaye mmoja ambaye ningeweza kumtaka shauri, ila namchukia." Mbona, hakika! Hakika, alimchukia, alikuwa nabii halisi. Akasema, "Yeye ni Imla, mwana wa Mikaya. Dhehebu lilimfukuza muda mrefu uliopita, halina ushirika wowote naye."

Kasema, "Hebu tumsikie."

"Loo," akasema, "namchukia."

Akasema, "Mfalme asiseme hivyo, lakini hebu tusikie anachotaka kusema."

Ndipo baadhi ya wazee wa jimbo wakakimbia huko, wakamwambia, kasema, "Maaskofu wote na kila mtu walisema *hivi* na *hivi*, huna budi kusema jambo lile lile."

Akasema, “Nitasema tu kile Mungu anachoweka kinywani mwangu.” Amina.

113 Loo, tunapaswa kuwa na Ndugu Zepp hapa sasa ili atuimbie lile pambio la *Amina*. Naam, bwana. Sema kile Mungu anachoweka kinywani mwako, kamwe hatasema chochote ila Neno Lake. Nabii ni msema kimbele, sawasawa na mtabiri. Kweli.

114 Kwa hiyo akasema, “Nitasema yale Mungu asemayo.” Ndipo akachunguza ono lake, kasema, “Hebu nichukue usiku wa leo, nione kile Bwana asemacho.” Kesho yake asubuhi, akatoka na alikuwa na BWANA ASEMA HIVI.

115 Kwa nini? Alilichunguza, alijua ya kwamba nabii huyo halisi aliyemtangulia, ambaye Neno la Bwana lilimjia, ilibidi awe sahihi. Alimlaani Ahabu, akamwambia mbwa wangeilamba damu yake, naye Yezebeli atatapanywa mashambani, na kadhalika. Alijua hakuna chochote chema kingeweza kutoka katika kitu hicho, alikuwa mnafiki.

116 Nitawaambia, ya kwamba Mungu kamwe hatalibariki kanisa maadamu linajiundia dhehebu na kujiweka upande mmoja, ambao Mungu amethibitisha kote katika wakati amelaani. Nionyeshe kundi moja la watu ambapo Mungu aliinua uamsho kupitia kwa Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Lutheri, Wakampbeli, lolote lile. Wakati alipoinua kundi la watu na kuanzisha uamsho, walipojiundia dhehebu walikufa wala hawakurudi tena. Mungu anawezaje kubariki alichokilaani? Loo, rudini, Louisiana! Mwaka wa Yubile unaendelea, rudini makwenu, rudini kwenye Urithi wenu. Hakika.

117 Angalieni, ndipo akapanda huko mlimani na kupoteza uhai wake, kwa sababu tu hasa, angalieni, ya kwamba Mikaya alisema unabii wake naye alijua ya kwamba ono lake lilikuwa sawasawa kabisa na Neno la Bwana. Bila shaka.

118 Imetufanyia nini? Imefanya jambo lile lile. Tulichukua wingi wa mashauri kwa ajili ya usalama, huo unaenda katika sehemu nyingine ya Maandiko, naweza kusema, “Yuda alienda akajinyonga nawe nenda ukafanye vivyo hivyo.” Lakini ha—halitumiki vizuri katika Maandiko; huna budi kulifanya liseme vile hasa linavyosema, si la kufasiriwa apendavyo mtu yeyote, lisome jinsi tu linavyosomeka. Hivyo ndivyo linavyopaswa kuwa, ndipo basi sikuzote utalirudia na Mungu hana budi kuliheshimu, Yeye huliangalia Neno Lake ili kutimiza ahadi Zake.

119 Imetufanyia nini? Ilidhoofisha imani yetu, jambo la kwanza. Nina orodha ya mambo yaliyoandikwa hapa, kurasa kumi, kile ambacho imetufanyia, nitaruka sehemu yake. Jambo la kwanza, ilidhoofisha imani yetu kwa sababu ilitutenganisha, nasi tukamwona ndugu mwingine katika dhehebu lingine akinena kwa lugha, na kumpokea Roho Mtakatifu, na kufanya mambo yale yale tuliyofanya, na hata hivyo tulifundishwa

kwamba yeye ni maskini mnafiki kwa sababu hakuamini katika kundi letu. "Hatujagawanyika, sisi sote ni mwili mmoja; mmoja katika tumaini na mafundisho," Bibilia, "mmoja katika upendo." Ilidhoofisha imani yetu, ikatupoozesha. Naam, bwana.

120 Ilifanya nini? Ilifanya kuku kutoka kwa tai, ndege wa ardhini kutoka kwa wale wa Mbinguni. Vema, ku—kuku ni ndege kweli, lakini yeye ni wa ardhini, yeye huweka kiota chake hapa chini ambapo kila paa anayekuja, anayekaribia, huvunja mayai yake na kuwachukua vifaranga wake na kadhalika, lakini si tai, yeye hukijenga juu sana kule mpaka hakuna kitu kinachoweza kumgusa.

121 Mungu anafananisha urithi Wake na tai, mnajua. Hiyo ni kweli. Nasi tuna kundi la kuku wa Kipentekoste wala si tai. Ni nini kiliifanya? Tunawapa chakula cha kuku, hiyo ndiyo iliyosababisha hilo, namna fulani ya kanuni za imani ama dhehebu, si Neno la Mungu aliye hai. Tulilivuta kwa nguvu, na kuligeuza, na kufanya kile tulichotaka kufanya kutoka kwalo kuunda dhehebu, tukaongeza mafundisho ya sharti sawasawa na vile kanisa la Kirumi lilivyofanya, jambo lile lile. Si ajabu alikuwa mama wa makahaba.

122 Naam, bwana, wanawapa chakula cha kuku, kanuni za imani ya kimadhehebu, nao wameishi kwa hicho, hicho ndicho chote wakijuacho. Wao ni watu wa ardhini, hawajui jinsi ya kuinua miguu yao, na kuinuka katika Uwepo wa Mungu, na kudai ushindi, hawajui jinsi ya kupaza sauti kuziimba sifa za Mungu, hawajui jinsi ya kukubali uponyaji wa Kiungu. Unazungumza nao, wanalia kama nyumbu, hawajui lolote kuhusu hilo. Mimi si...Ikiwa mimi...Nisameheni tu ikiwa nimesema kitu kibaya. Sikukusudia kusema chochote kibaya, namaanisha kutoa hoja kwamba watu, unaweza kuzungumza juu ya uponyaji wa Kiungu, wanageuza mgongo wao, loo, hata makundi yetu ya Kipentekoste yanaukana.

123 Je, mnajua Kanisa Katoliki la Kirumi lilikuwa ndilo kanisa la kwanza la Kipentekoste? Miaka elfu mbili imeliletea hayo, acha dhehebu hili la Kipentekoste liendelee jinsi limekuwa, katika miaka mia moja kutoka sasa litakuwa baya zaidi kuliko kanisa la Kirumi, hivyo ndivyo kuongeza kanuni za imani na mafundisho ya sharti kunavyofanya, unawafanya kuku badala ya tai.

124 Mungu—Mungu ni Yehova-Tai, hawa watoto wote ni tai wadogo. Ndugu, wao wanajua jinsi ya kupanda huko juu angani juu ya kila namna ya vitu vya fito hapa chini vinavyoendelea, hawataki makusanyiko yenu ya vibandani, wanaruka juu mbinguni kuliko na nyota, wanapumua hewa safi ya usafi. Naam, bwana. Loo, naam.

125 Wamefanya makusanyiko yetu kuwa ya kisasa, hivyo ndivyo walivyofanya, na jambo jingine ambalo wamefanya, wameleta

utovu wa uadilifu kwa wanawake wetu. Kweli kabisa. Wanaume wetu, ndugu zetu, wamewaweka katika madhehebu na kusema, "Usiponinii . . . Kama tukiitoa . . . tutakunyang'anya kadi yako, kadi yako ya ushirika, mbona, kamwe hutaweza kumhubiria mtu mwingine yeyote kwa sababu tutakuondosha . . . tutakutenga," nao wanaogopa, hilo linamfanya kuku.

126 Ndugu, jiachilie, rudi. Hii ni yubile, wewe ni tai; mtu yeyote asikwambie wewe ni mwewe, au, kuku, samahani, ya kwamba wewe ni, vema mwewe pia, na koho, naam, bwana, wewe ni tai. Naam, bwana. Hujali kanuni za kale za imani na madhehebu yaliyokufa. Hebu turudi, sisi ni tai, tunarukia mbinguni. Amina.

127 Tai anaweza kwenda mahali ambapo hakuna ndege mwingine anayeweza kuwazia kwenda, kama angejaribu kumfuata, angesambaratika, yeye ni ndege aliyeumbwa maalum, kweli kabisa. Nawaambia, mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu ni mwanamume au mwanamke aliyeumbwa kimaalum. Haleluya! Wamezaliwa na Roho ndani yao anayejua jinsi ya kutenda na kufanya na kuwa mwana wa Mungu. Amina. Ni kweli. Unajua hiyo ni kweli.

128 Naam, bwana, sio lazima tuwe na . . . Wanawake wetu, ilikuwa ni aibu kwa wanawake wetu kukata nywele zao, wanafanya hivyo; ilikuwa ni makosa kwa wanawake kujipodoa, wanafanya hivyo, Wapentekoste. Nilikwenda, hapa si muda mrefu uliopita, kwenye mojawapo ya makanisa yetu maarufu ya Kipentekoste, walijua yaliyokuwa yanakuja, kwa hiyo nikaanza tu kulihubiri Neno. Nami nilipokuwa nikilihubiri, karibu kila mmoja wao aliamka na kutoka nje, karibu hawakuwa wa kutosha kufanya shule ya Jumapili, wakatoka wanawake waliokatwa nywele, akina Riki na Elvis, na wote wakiondoka kwa njia *moja* na njia *hii*, njia *ile*, nao walikuwa walimu wa shule ya Jumapili. Nikasema, "Kundi hilo la kuku, hawawezi kustahimili nyama nzuri safi." Hiyo ni kweli. Tunahitaji Roho Mtakatifu. Tai hula Chakula cha tai, tai hawaishi kwa kanuni za imani, wanaishi kwa Roho Mtakatifu, wanaishi kwa Kristo, tai halisi wa Mungu, wao, hawana budi kuzaliwa maalum.

129 Kuku anasema, "Mimi pia ni ndege." Najua wewe ni ndege, hiyo ni kweli, lakini sio tai. Hawalisikii, hawawezi kulivumilia, hawawezi kulipata, kujazwa, kamwe hawawezi kulichukua. Kwa nini? Hawawezi kulichukua, hawajui lolote juu Yake. Wameyarasimisha makusanyiko yetu, wakayapoozesha, makusanyiko yetu yamelemazwa na mambo ya kisasa; tuna makanisa makubwa mazuri sana, madhehebu makubwa mazuri sana, madaktari wazuri sana mashuhuri wa mambo ya kiungu.

130 Kama nilimheshimu maskini mwanamke mmoja wakati mmoja, alikuwa Bibi McPherson, mke wa Rolf McPherson, maskini Mkristo mzuri sana. Nami nilikuwa nimeketi, nikizungumza, kwenye kiamshakinywa pamoja na mmoja

wa wafanyabiashara Wakristo nasi tulikuwa tumeketi pale tukizungumza, tukiwa na, loo, kilikuwa ni chakula cha jioni, naam. Na kwa hiyo, Ndugu Teeford akaniambia, akasema, “Ndugu Branham, nashangaa ni kwa nini hujaja kutuona.” Muda mrefu uliopita. Naye Dada McPherson, alitoka katika nyumba ya Kipentekoste ya mtindo wa kale, baba na mama yake, mmoja wa waanzilishi wa kale wa Pentekoste.

131 Nami nikasema, “Vema . . . ” Wakaanza kuzungumza kuhusu ndugu mwingine aliyeanzisha kanisa kubwa na kuwachukua karibu wote waliokuwa kwenye hilo hekalu, wote aliokuwa amefanya *hivi*. Nikasema, “Vema, hizo ni sifa duni sana kwa kanisa hapa, kama wataenda kule kujenga kanisa la dola milioni moja na wanalo moja lililojengwa hapa tayari.” Nikasema, “Watoto wenye njaa hula huko nje kwenye pipa la takataka, wana njaa. Hivyo tu.”

132 Basi tulipoanza kulizungumzia, Dada McPherson alisimama na kusema, “Rolf, hiyo ni kweli.” Akasema, “Tuna nini hapa ila mzigo wa dola milioni moja usio na faida?”

133 Nikasema, “Kama mngerudi kwenye Injili hiyo ambayo Bibi McPherson aliitetea, kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu na uweza wa Mungu badala ya Daktari, Ph.D., LL.D., namna hiyo yote ya elimu hapa . . . ” Tunahitaji kurudi kwenye Pentekoste, kurudi kwenye Injili, kurudi kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Nenda huko nje ukawaone hao wahubiri wanawake, nywele fupi zilizokatwa, kila namna, mnajua jinsi wanavyofanya.

134 Mnajua linavyofanya? Nilienda hivi majuzi hapa nchini, na kamwe sikuona . . . Nilimwona mwanamke hapa Los Angeles, mimi, nikipanda kwenda kumwombea, nilidhani alikuwa na ukoma, lakini nilikuwa nimeona ukoma, haukufanana hivyo, kijani kibichi chini ya macho na kila kitu namna hiyo. Mimi . . . Kile . . . Mimi kamwe . . . Nilianza kupanda na kusema, “Mama, mimi ni mmishenari, nimeona ukoma, nimeona upele mbaya, nimeona kila kitu, sijapata kuona kitu kama hicho, mimi ni mhudumu, ungeniruhusu nikuombee?” Huyu hapa mwingine akaja, alifanana naye kabisa nami nikawazia, “Ngoja kidogo.”

135 Ilikuwa ni nini? Mbona, ni aibu! Labda mwanamke mrembo, lakini unajua hupaswi kuonekana kama kioja, kitu *fulani* cha zamani za kale, kitu *fulani* kutoka mahali fulani wanapoita Marsi, wewe ni mtakatifu wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili, kaa jinsi Mungu alivyokuumba, kweli, wengi wao wanawake wa Kipentekoste. Wakati mwanamke anapofanya hivyo, bandia kwa nje, upande wa nje huonyesha tu kile kilicho ndani, kule ndani ni bandia. Ana dhehebu bandia analoshikilia badala ya . . . Kristo anapaswa kuyajaza maisha yake kwa nguvu za kufufuka Kwake, badala yake, amechukua kanuni fulani za imani za

kujibunia. Nje daima huonyesha kilicho ndani, mti hujulikana kwa matunda uzaayo. Loo, jamani!

136 Najua mnaweza kufikiria mimi ni mkosoaji, lakini mimi si mkosoaji, ninajaribu tu kuwaambia kilicho kweli. Angalieni kile kimeyafanya makanisa yetu siku hizi, angalieni tulipo. Mbona, mama zetu hawangewazia kitu kama hicho, ndugu zetu wasingewazia kitu kama dhehebu. Kwa nini . . . Ungalirudi kule katika siku zake za mwanzoni na kusema jambo kama hilo, wangekucheka usoni pako, tungesema, "tulitoka kwenye matapiko hayo, tulitoka kwenye kugaagaa huko, Mungu alituita tutoke."

137 Hatutaki kurudi, kama Israeli, kwenye vyungu vya nyama tena vya Misri, Mungu alitutoa humo, lakini tumekuwa tukitaka kurudi. Tulirudi, mnaweza kuona kile tulichopata, kitu kile kile walicho, chungu hakiwezi kusema kuwa birika ni nyeusi. Hiyo ni kweli. Sita ya dazani moja na nusu ya hiyo nyingine. Kanuni za imani na kadhalika zilitutenganisha tu. Lakini ndugu, loo, ningeweza kushikilia hili kwa muda mrefu, lakini hebu tusifanye hivyo. Hebu niwape habari moja njema: Huu ni mwaka wa Yubile. Ikiwa mmejichanganyisha katika mambo ya aina hiyo, hima turudi, tunao Urithi.

138 Baba wa Pentekoste walipiga vita wapate tuzo, nao wakasafiri katika bahari zilizojaa damu, tusitembee kwenye kitanda hiki cha maua ya urahisi kwa kujiunga na dhehebu fulani, na kutulia, tukisema, "Mungu abarikiwe, mimi ni Mpentekoste."

139 Hebu tupate tukio, tumrudie Mungu, na turudi kwenye Chakula cha tai, hebu turudi kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu, hebu turudi kwenye Neno la Mungu, hebu turudi kwenye kufunga-na-kuomba.

140 Mbona, kanisa lilisahau mikutano ya mtaani zamani sana, kanisa lilisahau usiku wake mrefu wa maombi. Mbona, hawawezi kuomba dakika kumi na tano tena, loo, jamani, na wanapoomba, ni jambo dogo rasmi, nusu yao wanashikwa na usingizi. Mbona, ni—ni—ni fedheha! Kuku wakijaribu kula Chakula cha tai, huwezi kufanya hivyo, hakitameng'enywa. Hiyo ni kweli. Hujaumbwa kwa ajili ya Hicho, hujaumbwa kwa ajili ya sehemu inayoparuza, huna budi kuumbwa mgumu, na njia pekee unayoweza kupata hiyo ni kuzaliwa mara ya pili na kubadili njia yako na kurudi. Amina. Naam, bwana. Naam, bwana, ni wakati wa kurudi.

"Kurudia kitu gani, Ndugu Branham? Kurudi kwenye dhehebu nilimotoka?"

Hapana, rudi kwenye Urithi wako, Urithi ambao Baba yetu alituachia.

"Alifanyaje . . . Aliacha Urithi wa aina gani?"

"Ngojeni ninyi, katika mji wa Yerusalemu, hata mtakapovikwa Uwezo utokao Juu." Huo ndio Urithi.

141 Sio, "Nenda, kajiunge na *hili*, na nenda ukajiunge na *lile*, nenda ukajiunge na *hili*." Ngoja hata Nguvu zishuke kutoka Juu. "Muda gani?" Mpaka. "Siku moja? Siku mbili?" Ngoja mpaka. Usichukue hisia kidogo, fadhaa kidogo, ngoja hapo mpaka utakapokufa na kuzikwa na kuzaliwa upya katika Kristo Yesu, na kila pigo la maisha yako linadunda Yesu Kristo, mpaka uweze kuona Maisha ya Kristo yakiakisiwa moja kwa moja ndani ya ma—maisha yako, jinsi unavyoenenda, naam, bwana, mpaka unapoweza kupata Nguvu hizo kama walizokuwa nazo hapo mwanzo.

142 Rudini kwenye Urithi wa Kipentekoste. Naam, bwana. Hiyo ndiyo Mali yako, dhehebu siyo mali yako, Pentekoste ndiyo Mali yako, sio dhehebu la Kipentekoste, baba zenu walitoka katika kitu kama hicho, Tukio la Kipentekoste ndilo Milki yenu. Tujichunguzeni. Kupigwa kwa Baragumu, "Baragumu ya aina gani?" Neno, Baragumu ya Mungu, Roho Mtakatifu katika Neno.

Loo, mshairi alilielezea vizuri wakati aliposema:

> Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
> Ishara walizotabiri manabii;
> Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
> Rudini, enyi mliotawanyika makwenu.
>
> Siku ya ukombozi imekaribia.
> Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
> Jazweni na Roho, taa zenu zikiwa zimesafishwa na ni safi,

143 Leo, tunao wahubiri, waadilifu, wenye elimu, wasomi wazuri, waliojitokeza, wanaoweza kusimama na kamwe wasijongee, wasivuruge unywele, wasitoe hata tone moja la jasho, nao wanasimama tu hapo na kuzungumza, na, loo, wanatoa vikorokoro vya kanisa na kila kitu kikipendeza sana kwa dakika kumi na tano huku mnalala, mnarudi nyumbani, na kujiita Wapentekoste.

144 Ndugu, tunahitaji maskini mhubiri wa kale wa mwituni ambaye atajitokeza amevalia ovaroli na kuingia mimbarani (Haleluya!), akiwa ametiwa mafuta kwa nguvu za Mungu, hatahubiri dakika tano kabla Roho hajalichukua kanisa, nalo limepaa mbinguni usiku uliosalia, ni tai, hawatadonoadonoa vitu vya kitaluni, wanapanda mbinguni kwa ajili ya Chakula chao.

145 Kupigwa kwa baragumu, naam, bwana, rudini, mliotawanyika. Lakini kama mliuza urithi wenu, kama mliuza na kufanya mambo haya (Ninasema nini? Rudini!) ikiwa ulijiunga na dhehebu fulani linalojaribu kukuweka mbali na ushirika na ndugu wengine, achana na kitu hicho, hii ni

yubile. Amina. Najisikia kubarikiwa. Rudini. Rudini! Hii ni yubile, usiiache ipite. Kumbuka: Usiache ipite. Kama umejiuza, kama umeingia ulimwenguni, kama umetenda dhambi, ulijua ya kwamba wakati mmoja ulikuwa na hilo tukio, ulienda na kujiunga mahali ambapo huwezi kushirikiana na hao wengine, umefanya mambo haya yote, sijali ulichofanya, kama wewe ni mwana, una haki ya kurudi sasa kwa sababu ni yubile, ni wakati wa yubile.

146 Lakini kama ulitulia tena ukutani mahali fulani, ukaweka jina lako chini na kutia nanga, *ukafanywa kuku* kabisa, hakutakuwa na mengi yatakayokupata, maana hutawahi kuisikia. Utatoka nje na kusema, "Vema, nadhani ilikuwa ni sawa, nimesikia hilo hapo awali." Unaona? Nenda nyumbani, ulale, uamke kesho yake asubuhi; lakini hulali ukaitoa imani, Neno la Mungu, huwezi kulitikisa likatoka, kama wewe ni tai, umeshika kitu fulani.

147 Hii inasikika kuwa ya kukufuru, nami natumaini... silimaanishi hivyo kwenu, bali si—silimaanishi mwenyewe. Kama yule mkulima aliyeweka kuku, alikuwa na, hakuwa na, vema, alikuwa na mayai ya kutosha kumweka, kasoro moja, akaweka yai la tai chini yake. Wakati maskini tai huyo alipozaliwa, alikuwa ni kitu cha kuchekesha kuliko vyote miongoni mwa hao kuku ulichopata kuona, yeye ni ndege wa kipekee, vema. Hivyo yeye...Maskini kuku angelia naye angekula, na karibu chochote, naye maskini jamaa huyo, huo haukuwa mlo wake, alininii tu—kamwe asingeweza kuuvumilia. Naye angesikia mlio huo, kuku. Hiyo ina maana gani? "Tuna karamu za sambusa, mikutano ya kijamii, madansi, karata." Mnaona? Yeye ni tai, asingeweza kabisa kuelewa mambo hayo.

148 Siku moja, maskini mama yake, akimtafuta, lazima ulikuwa ni Mwaka wa Yubile kwa jamaa huyo mdogo, maskini huyo mama akaja huko na kupaza sauti, akaangalia juu, kasema, "Huo unasikika sawa." Alisikia kitu fulani.

Akasema, "Mwanangu, wewe si kuku, wewe ni tai, toka humo."

Kasema, "Mama, nitatokaje?"

149 Kasema, "Pigapiga tu mabawa yako, huo ndio ukombozi wako uliopewa na Mungu. Umezaliwa tai, una urithi. Njoo huku juu zaidi, ondoka kwenye upuuzi huo. Rudi!"

150 Akapigapiga mara nne ama tano, na alipofanya hivyo, aliketi moja kwa moja kwenye nguzo uani, moja kwa moja katikati ya dhehebu la Kipentekoste. Akasema, "Mwanangu, itabidi uruke juu zaidi ya hapo la sivyo siwezi kukupata." Mruko uliofuata akaangukia kwenye mbawa za mama yake na kwenda mbinguni. Huo ndio wito wa siku hizi, ndugu. Rudini. Nyinyi si kuku, ninyi ni tai. Rudini. Naam, bwana. Sasa, tunajua ya kwamba ni kweli.

151 Sasa, Baragumu inalia, Inatoa sauti, huu ni mwaka wa hamsini. Mlisikia kwa mzee huyu wetu asubuhi ya leo na kupitia jumbe hizi jinsi ilivyokuwa. Ninawaambia usiku wa leo kwamba ahadi ni sasa, hebu turudi. Paulo alisema katika Matendo, na hapana, katika Wakorintho wa Kwanza 14:8, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani awezaye kujitayarisha?"

152 Tunao watu mashuhuri wanaovuka ulimwengu siku hizi, makanisa yote yakiungana kama mtambo mkubwa wa kisiasa, watu wanatokea kama utawala fulani mkuu, wakija kwake, na muda si muda mwajua, Wamethodisti wanachukua wao na kwenda *huko*, nao Wabaptisti wanachukua wao na kwenda *huko*, na mmoja hajui anachofanya huyo mwingine.

153 Masalaale, sivyo ilivyo. Baragumu inatoa sauti isiyojulikana, "Njoo, ujiunge na kanuni hii ya imani, njoo, ujiunge na kanuni ile ya imani," huku Biblia inasema jambo lingine. Naam, bwana, ikiwa tarumbeta haitoi sauti inayojulikana, huwezi, hujui ujitayarishie nini.

154 Lakini unapoona Baragumu ya Mungu ikitoa sauti ya Neno la Mungu, na Mungu akiithibitisha kwa ishara na maajabu kama alivyosema angefanya, hiyo ni kweli. Na ikiwa baragumu itatoa sauti isiyojulikana, Kapteni Mkuu hatathibitisha wito huo. Loo, ndugu, hilo lilikuwa la kulishibisha tumbo! Kapteni Mkuu hatathibitisha wito huo. Kwa maana alisema katika Marko 16, "Ulimwenguni mwote; na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Huyo ni Kapteni Mkuu. "Kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya." Haleluya! Huo ndio wito. Kapteni alisema, "Nitawathibitisha kwa hili." Alisema pia katika Yohana 14:12, Kapteni Mkuu alisema, "Aniaminiye Mimi," si yeye asemaye anaamini, "yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Amina. Hiyo ndiyo sauti inayojulikana.

Aliwaambia . . . Wayahudi hao, walisema, "Mbona, wewe ni mwanadamu unayejifanya Mungu."

155 Akasema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu basi msiniamini Mimi." Amina! Acha tuwe nazo, sisi ni kanisa. Utukufu! Kweli. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

156 Huku na huko kupitia Louisiana katika mkokoteni, katika gari kuukuu la Fordi Muundo wa T huku matairi yamefungwa kwa waya wa kufunga robota, walikwenda baba zenu wakihubiri hilo, dhidi ya mafundisho haya ya sharti mliyoongeza kwake. Tokeni kwake. Rudini. Rudini. Tubuni. Rudini mlikotoka, huu ni mwaka wa yubile. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Naam, bwana.

157 Loo, hebu niseme hivi! Hii inarekodiwa, najua. Enyi kanisa tajiri la Laodikia, mlisema, "Sina haja na kitu." Mnajua Biblia ilisema mtakuwa hivyo, kasema, "Wewe ni vuguvugu."

158 Loo, mnasema, “Tunapaza sauti na kumsifu Mungu.” Loo, naam, Israeli walifanya vivyo hivyo, nao wakafanya kosa baya sana, na hilo silo. Ninamaanisha ile bidii motomoto ya Mungu, hakuna kinachoweza kuizuia. Angalieni hiyo Waebrania 11 pale ambapo kwa mtikiso mmoja tu wa kichwa wa hao wazee kutoka kwa Mungu, walishinda milki za wafalme, wakatenda haki, wakafunga kinywa cha simba, na wakaepuka moto, na mambo waliyofanya kwa imani kwa mtikiso mmoja tu wa kichwa kutoka kwa Mungu.

159 Siku hizi Mungu anaweza kutuma mhubiri na kutwanga Neno hilo kwa nguvu awezavyo, nasi tunashikwa na usingizi, tunasimama na kutoka nje. Si ajabu mmezingirwa kwa ukuta, kanisa limezingirwa. Mimi ni . . . Najua hii inarekodiwa, inaenda sehemu nyingi sana, mnaona, hii, inaenda ulimwenguni kote, kwa sababu tuna mauzo ya kanda kote ulimwenguni, inaenda kufanya umishenari katika nchi za kigeni.

160 Nami ninamaanisha kila mtu. Naam, bwana. Rudini. Huu ndio wakati wa kurudi wakati wito unapokuja. Naam, bwana, ishara hizi zitafuatana na wana, sio watumwa, si watumwa waliofungwa, si watumishi, bali wana. “Ishara hizi zitafuatana na waaminio; na hakuna mtu awezaye kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu.” Hiyo ni kweli. Unaweza kusema unamwita, lakini Roho Mtakatifu hana budi kulithibitisha na kulihakikisha. Naam, bwana.

161 Loo, Laodikia tajiri yenye kanisa upande wa nje, Kristo akiwa nje ya kanisa, hasa, akibisha, akijaribu kuingia, kasema, “Mimi ni tajiri wala sina haja na kitu.”

162 Hakika, unakuja moja kwa moja na Wamethodisti na Wabaptisti, ukawashinda kwa idadi, lakini ziko wapi hizo nguvu za Mungu zilizoshuka miaka hamsini iliyopita? Iko wapi ile bidii iliyowaka mioyoni mwa hao watu waliotembea kwenye njia za reli na kuokota mahindi na kuyasaga huko nje wapate kuileta Injili? Tunawafanya wapinduke kwenye makaburi yao. Tunaleta fedheha kwa baba na mama zetu waliopiga vita wapate kushinda tuzo. Na hapa *tunajiburudisha* kwenye ninii ya kimadhehebu . . . Je, nimesema ya kutosha kuwafanya mfahamu, ni kurudi?

163 Mungu alilivuta Kanisa Lake teule kutoka katika hayo madhehebu miaka hamsini iliyopita. Mungu, wavute hao masalio! Hii ni yubile, Yeye anaita tena. Rudini, yubile! Miaka hamsini iliyopita Mungu aliwatoa humo, na usiku wa leo anajaribu kufanya jambo hilo tena. Tutaendelea kesho usiku, imepita na robo. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

> Mataifa yanavunjika, (Kristo yuko kila mahali.) Israeli inaamka, (Ni taifa lake lenyewe, lina pesa zake lenyewe, jeshi lake lenyewe, liko katika Umoja wa Mataifa.)
> Ishara ambazo Biblia ilitabiri;

Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu, (Mabomu ya atomiki na kila kitu.)
Loo, rudini, Enyi mliotawanyika makwenu.
(Huu ni mwaka wa yubile.)

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zikiwa
zimesafishwa na ni safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

164 "Rudini. Rudini." Roho Mtakatifu analia, "Rudini!" Ninaweza kuwazia wakati Yesu alipotazama nje juu ya Yerusalemu naye akalia, aliipenda, nao walikuwa wamemkataa. Na mtu ambaye amejazwa na Roho usiku wa leo anaweza kuangalia nje juu ya kanisa na kuwaona watu wanaopaswa kung'aa kwa uweza wa Mungu wenye utukufu, huku Roho Mtakatifu ndani ya moyo wako akilia machozi ya majuto. Tumefanya nini?

165 Mungu alituita sisi, baba zetu watoke miaka hamsini iliyopita, nasi tukarudi. Nanyi mnaona kilichotuletea: kundi la aibu chini ya jina la Pentekoste, watu wanaovuta sigara, kunywa pombe, waliooa mara tatu au nne, wanawake wanaokata nywele zao, kujipaka rangi, kutumia ninii zao...kaptura, wanavaa mavazi ya kizinifu, kila kitu, wanajiita dada wa Kipentekoste. Ni fedheha jinsi gani kwa Jina la Kristo! Ni fedheha jinsi gani juu ya Kanisa Lake! Si ajabu anasema majina yanayokufuru yalipatikana Babeli, dhehebu, machafuko, yote yamevurugika, kila aina ya hili, lile, na linginelo. Kristo yuko wapi katika jambo hilo lote? Rudini, enyi watu.

166 Ninashangaa usiku wa leo, wakati tumeinamisha vichwa vyetu, watu wanaamini huu ndio ukweli, kwamba tunapaswa kurudi wakati wa hii yubile, ni wito wa mwisho wa Mungu kwa Kanisa Lake, kama mnaamini, inueni mikono yenu kwa Mungu na mseme, "Mungu, nataka kuja," inua tu mkono wako, useme, "Ninaamini, ninaamini," tai wote sasa wanaojua na kuamini.

167 Baba yetu wa Mbinguni, unaona mikono hii, angalau nusu ya kusanyiko hili au zaidi wameinua mikono yao juu, na wanajua kwamba ni kweli. Mungu wa Mbinguni, mtume Roho Mtakatifu, Bwana. Ninaona majira yanazidi kuingia giza, na mioyo ya watu inakua, inazidi kuwa baridi na rasmi, makanisa yamepotea, lakini hawajui ile bidii na upendo na nguvu walizojua miaka hamsini iliyopita katika mwenendo wa Kipentekoste, wamejifanyia mapango madogo, wamejizungushia kuta pande zote, nao hawawezi kutoka katika yubile, haikuwa hivyo kamwe.

168 Na Mungu, Wewe ni Mungu asiyebadilika, Unajidumisha Mwenyewe sawa siku zote, amri Zako haziwezi kubadilika, kila uamuzi ni mkamilifu, kwa hiyo, haupaswi kubadilishwa, ni mkamilifu, ni Neno Lako. Na iwe usiku wa leo, Bwana, jalia iwe

kwamba mtumishi Wako, kila mahali, watu wengi wanaomcha Mungu, Bwana, wanasimama siku hizi kote nchini, wakihubiri, "Rudini, rudini." Nyuso zao zimejaa aibu wahudumu wageni wanapoingia kanisani na kuwaona wanawake na wanaume na jinsi wanavyofanya na kutenda, na—na wahudumu waliojazwa na Roho, nao wanajua, nyuso zao zimejaa aibu. Wafanyeje? Wakisema lolote kuhusu hilo, mfumo huo wa kimadhehebu unawafukuza.

169 Ee Mungu, watoe hao tai kutoka humo, Bwana, watoe kwenye kizimba hicho, hii ni yubile, watoe uwalete kwenye uhuru na Roho Mtakatifu. Jalia wasimame, kufa kupona. Babu zetu walijitenga na Wamethodisti, Wabaptisti, na Walutheri, halafu kizazi baada ya kizazi ambapo walijiundia madhehebu, wakajiuza. Uliwaita tai Wako kutoka kwenye zizi hilo, kutoka kwenye hicho kitalu, Bwana Mungu, Wewe ni Mungu yeye yule usiku wa leo, ita tena, Bwana. Ni wakati wa yubile.

170 Jalia, Baba wa Mbinguni, kwamba kabla ya juma hili kwisha kwamba tutaona nguvu za Mungu zikirudisha tena ishara kuu na maajabu, jalia wagonjwa waponywe, viwete waondoke wakitembea, jalia vilema watembee, vipofu waone, viziwi wasikie, wafu wafufuliwe, na uweza wa Mungu udhihirike mioyoni. Lijalie.

171 Anzisha uamsho tena, Bwana, watoe watu katika mambo haya baridi ya kawaida wanayofanya, kucheza muziki kidogo na kucheza dansi, wanamwita Roho aingie, kwa mdundo wa muziki. Ee Mungu, mtakatifu wa Mungu angeweza kucheza huku na huko mitaani, ama kwenye chumba cha baa, ama pengine popote chini ya nguvu za Mungu anapocheza kwa Roho, na kupaza sauti na kumsifu Mungu. Wao. . .Huwafanya waishi tofauti kwa nje, Bwana, nalo kanisa Lako linaonyesha kile kilicho ndani yake, tupu, juu juu, kanuni za imani, dhehebu, wameliwa, wameoza, ugonjwa wa kufisha kila mahali, ni kidonda kitoacho usaha, hakika.

172 Ninaomba, Mungu, ya kwamba utapokea sadaka yangu usiku wa leo ninapoiweka juu ya Madhabahu ya dhahabu yenye ile Dhabihu, Kristo, aliyefundisha Neno. Nami ninaita usiku wa leo, Bwana, jalia Roho Wako alirudishe kanisa tena. Tujalie, Baba. Ninayakabidhi maneno haya Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Ninayakabidhi haya. . .kanisa Kwako, ninalikabidhi kundi hili la watu Kwako. Ee Bwana Mungu, tufanyie jambo fulani, naomba, yasikie maombi ya mtumishi Wako. Tujalie, Bwana. Ninaomba kwa uaminifu kwa moyo wangu wote katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

173 Mnampenda? Je, mnamwamini? Mnaamini ni saa ya kurudi? Tumechelewa sana kuanza ibada ya uponyaji sasa. Tutaipata kesho usiku. Imechelewa sana. Ninataka kushikilia hili kwa muda kidogo.

174 Mnafikiri mimi nina wazimu? Mimi si mwendwazimu. Mimi sija-. . .Ninajua hakika ninachozungumzia, najua ni kweli. Kanisa limeoza kabisa. Hiyo ni kweli. Linahitaji kuzaliwa mara ya pili, linahitaji kurudi kwenye Urithi wake, linahitaji kurudi kwenye Pentekoste, linahitaji kurudi kwenye jambo *fulani*.

Loo, unasema, "Mimi ni Pentekoste."

175 Loo, ndugu, naona aibu kujiita Mpentekoste, si kwa sababu ya jina takatifu la Pentekoste, lakini kwa sababu kwamba ningeweza kuwa tofauti. Ninataka kuyasalimisha maisha yangu mwenyewe, nataka kujiweka juu ya Madhabahu ya Mungu na kusema, "Bwana, nipige, na unifinyange, na unichukue mpaka niwe tofauti na nilivyo sasa, nifanye Wako na uniongoze, Bwana. Nimeongozwa sana na mwanadamu, nataka kuongozwa na Roho wa Mungu. Ninaungama, hii ni Pentekoste, ninataka kurudi tena kuona uamsho." Amina.

176 Je, mnaamini hilo? Hebu tuinue mikono yetu na kuimba, *Nampenda*. Tupeni sauti, dada, tafadhali sasa. Vema, kila mtu inueni mikono yenu na kuimba kwa sauti yako yote, *Ninampenda*, na tunapofanya hivyo, hebu tusimame kwa miguu yetu. Kwa pamoja sasa, onyesha ya kwamba unampenda Yeye, na tuwe Wapentekoste halisi.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

177 Sasa, hebu tuuvumishe. Sasa, kuna Mmethodisti amesimama karibu nawe, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mpentekoste, na tupeane mikono na kusema, "Mungu akubariki, Ndugu, hima turudi." Hebu tuseme hivyo tunapogeuka, tupeane mikono na kila mtu hapa.

> Na. . .

178 Hebu tuseme pamoja: "Hima turudi! Hima turudi! Hima turudi! Hima turudi!" Ndugu Holstein alisema, "Ulihubiri Mtaa wa Azusa hasa." Amina! Hima turudi!

> Nampenda, (Hebu tuinue mikono yetu.) Nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

Damu ya Yesu Kristo:

> Loo, mtiririko huo ni wa thamani,
> Unaonifanya mweupe kama theluji;
> Sijui chemchemi nyingine,
> Hakuna ila Damu Yake Yesu.

Sijui dhehebu lolote, sina deni lolote. Lakini ninawiwa yote na Yeye.

Yesu alilipa yote.
Ninawiwa Naye yote;
Dhambi ilikuwa imeacha doa jekundu sana,
Akaiosha ikawa nyeupe kama theluji.

Nampenda, (Hebu na tumsifu tu tunapoinua ninii yetu. . .) Nampenda, (Asante Baba, asante.)
(Naomba, Bwana, kwamba Wewe—kwamba Wewe utamtuma Roho Wako Mtakatifu.) . . . alipenda. . .(Ee Mungu, turudishe, Bwana, kwenye tukio hilo, umwage Roho Mtakatifu, juu yetu.)
. . .kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

179 Huku muziki ukiendelea, hebu tuendelee tu kuinua mikono yetu. Hebu tumpende tu, tumsifu tu. Hebu tuombe kwa njia yetu wenyewe, omba jinsi ufanyavyo kanisani. Wote wanaotaka kupata ubatizo mpya wasimame, pungeni mikono yenu huku na huko, "Nataka ubatizo mpya Bwana." Ee Mungu! Msifuni Yesu! Mungu, tuma Roho Mtakatifu juu yetu. Uturudishe, Bwana, kwenye matukio hayo tena, utusamehe makosa yetu, Bwana, na utusaidie kupata maarifa haya ya nguvu na ukweli wa Injili. Tujalie, Bwana.

wokovu. . .
Mtini Kalvari.

180 Papo hapo unaposimama, moja kwa moja kwa njia yako mwenyewe, papo hapo unaposimama, msifu tu Mungu, useme, "Mungu, nitakubali sasa hivi, ninakuahidi sasa hivi, kwamba sitaachilia hadi roho yangu irudi kwenye tukio la aina hiyo." Ni wangapi watafanya hivyo pamoja nami? Inua mkono wako. "Sitalegea, nitashikilia madhabahu."

Nampenda, na-. . .("Nitaomba! Nitaomba! Nitafanya chochote, Bwana, nirudishe kwenye—nirudishe kwenye urithi wangu, nirudishe mahali pangu halisi tena.")

. . .mimi (Mungu asifiwe!)
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

181 Loo! Jina la Bwana libarikiwe. Ee Mungu, tuma uwezo Wake. Watume manabii Wako, Bwana, watume pamoja na Neno, usiwaache wapatane juu ya jambo lolote. Rudisha kwenye Biblia, rudisha kwa Roho Mtakatifu, rudisha kwenye bidii; inua Kanisa lisilo na doa wala kunyanzi, Wewe uliliahidi, Bwana, uliliahidi, tunakuamini. Ninasihi kwa ajili ya kila mmoja wetu, Bwana, mimi mwenyewe pia. Utume, Ee Bwana. Tuma nguvu sasa hivi, jaza kila moyo. Ninaomba, Bwana, ya kwamba utatutumia kile tunachohitaji, Bwana, ulichomwaga

miaka hamsini iliyopita hapa katika jimbo hili. Imimine tena, Ee Bwana Mungu, jaza vitasa Vyako na kumwaga upendo wa Kristo mioyoni mwetu, na utufanye Kanisa hilo tunalopaswa kuwa, Bwana, ukitusamehe dhambi zetu.

182 Tunarudi usiku wa leo, Bwana, kama kundi la watu, tunarudi kama watu na mtu binafsi, tunarudi kwenye urithi wetu, Bwana, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mungu Mwenyezi, uliliahidi, lipe heshima, Bwana, lipe heshima Neno Lako, ninaomba katika Jina la Yesu.

Na . . . (Ee Mungu, Ee Mungu, utakatifu, haki,
urithi wa Mungu, hurithi sifa za watu Wake.)
. . . wokovu wangu
. . . Kalvari

183 Mnapoendelea kusimama, nataka huyu mzee wetu mpendwa wa imani . . . Jambo ambalo nimekuwa nikizungumzia, Ndugu, ni mambo ambayo nyote mliyapigania kwa miaka mingi iliyopita.

[Ndugu huyo anasema, "Kabisa."—Mh.]

Kanisa linapaswa kurudi kwenye jambo hilo, sivyo, Ndugu?

["Tumeondoka kutoka . . . Ili kuokoa huo mwenendo, inabidi turudi."]

Amina.

["Tumepitia njia ya madhehebu mengine yote, ilikuwa ni nzuri kwa kuanzia, ajabu, na hatua kwa hatua wameangukia kwenye makucha ya mitambo ambayo imekuwa ya kutengeneza watu wenye akili kuu. Hatuna budi kumrudia Roho, hatuna budi kurudi."]

Sikieni kilio cha mtakatifu huyo mpendwa mzee kutoka moyoni mwake huku machozi yakimtiririka usoni, anajua ya kwamba kuna nafsi zinazongojea ng'ambo ya madhabahu kule.

184 Yesu atakuja siku moja. Ninatumaini na kuomba ya kwamba Mungu atawainua wanaume, hapa, na wanawake ambao watarudi, ambao watarudi licha ya kila kitu. Rudini! Ni yubile! Ondokeni kwenye utaratibu huu, kamwe hamwezi kufanikisha chochote cha Mungu mle ndani, unakifanikisha tu kwa ajili ya dhehebu. Hebu tujitokeze na kufanikisha kwa ajili ya Mungu, na unaweza tu kufanya hivyo kwa Utaratibu Wake, Roho Mtakatifu, Huyo ndiye tuliyepewa. Mungu awabariki.

62-1122 Kurudi Na Yubile
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org